**KIJITABU CHA KUELIMISHA WAWEKEZAJI**

**KIMETAYARISHWA KWA USHIRIKIANO WA SOKO LA HISA NA HATI ZA DHAMANA (NSE) NA CHAMA CHA KENYA CHA MADALALI WA HISA NA BENKI ZA UWEKEZAJI (KASIB)**

**KIJITABU HIKI HAKIPASWI KUUZWA**

**KIJITABU CHA KUELIMISHA WAWEKEZAJI**

**'Hali ya hatari hutokana na ukosefu wa ufahamu kuhusu unalolitenda'– Warren Buffet**

**'Maarifa humfanya mtu kuwa bora zaidi' – Ralph Waldo Emerson**

**Kanusho**
Juhudi mwafaka zimefanywa kuhakikisha kuwa habari zilizotolewa kwenye kijitabu hiki ni kamilifu na sahihi. Hata hivyo kwa vyovyote vile chama cha KASIB hakitawajibika kumlipa mtu yeyote fidia kwa uharibifu unaotokana na matumizi ya habari zilizochapishwa katika kijitabu hiki wala hakitadhamini utoaji wa nakala za maelezo ya kijitabu hiki kwa kuwa ni sahihi, kamilifu na aminifu

Habari za kijitabu hiki haziendelezi ushauri unaohusu maswala ya uwekezaji, ushuru au sheria miongoni mwa maswala mengine.

Wasomaji wa kijitabu hiki wanashauriwa kuwasiliana na madalali au benki za uwekezaji kwa mapendekezo yoyote kupitia anwani zao zilizochapishwa kwenye kijitabu hiki katika ukurasa wa mwisho.

**Taarifa ya mwenyekiti**

**TAARIFA YAKE MWENYEKITI WA CHAMA CHA KASIB**

Chama cha Kenya cha madalali wa hisa na benki za uwekezaji ni chama kinachowakilisha nia na malengo ya kampuni za udalali wa hisa na benki za uwekezaji zilizo nchini Kenya.
**Wanachama wa chama cha KASIB wanadhibitiwa na halmashauri ya masoko ya mtaji (CMA), Soko la hisa na hati za dhamana la Nairobi (NSE) na kanuni za maadili bora ya KASIB. Kila mwanachama anatakiwa kufuata maagizo hayo.**

Chama cha KASIB kilizinduliwa kwa lengo la kutimiza maadili bora na kuendeleza viwango vya juu vya kitaaluma katika sekta ya masoko ya mtaji nchini Kenya.
Chama cha KASIB hutekeleza wajibu wake kwa ustadi wenye mwelekeo bora wa ukuaji kupitia mashauriano ya kila mara na washikadau wengine kwa kuangazia mbinu mwafaka zinazochangia kuimarika kwa sekta hii.

Chama cha KASIB kimekuwa na kitaendelea kuwa katika mstari wa mbele kuhimiza kuwepo kwa soko la mtaji lenye uthabiti na umaarufu. Aidha chama cha KASIB kila mara kimekuwa kikilenga mbinu bora za kuimarisha uanachama wake na kisha kuchangia pa kubwa katika ustawi wa sekta hii.

Mbinu kama vile kuelimisha mwekezaji, usimamizi bora na kuendeleza maadili bora ya kikazi ni baadhi ya maswala chama cha KASIB kinalenga kupigia debe.

Wawekezaji nchini Kenya wanalenga sana soko la hisa.
Kjitabu hiki kimetayarishwa ili kutoa mafunzo ya kina kuhusu soko la hisa na kuwawezesha wawekezaji kuelewa maneno magumu yanayotumika na jinsi soko hilo linavyoendesha shughuli zake.

Hatua hii inatokana na maombi kadha wa kadha kutoka kwa wawekezaji ambao wametaka juhudi za kuanzishwa kwa mpango wa ufafanuzi wa maswala magumu wanayokumbana nayo kwenye masoko ya mtaji kuzinduliwa.

Mshauri wako wa maswala ya uwekezaji yuko tayari kutoa mwangaza zaidi kwa maswala utakayohitaji ufafanuzi

zaidi.

Kadhalika waweza kuwatafuta wakufunzi wetu ambao hivi karibuni watazuru kote nchini katika shule na miji na kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na wawekezaji.

Kijitabu hiki ndicho cha kwanza kutolewa katika msururu wa jarida zitakazochapishwa na KASIB kwa ushirikiano wa NSE katika kipindi cha majira ya wastani na katika muda mrefu ujao.

KASIB kwa ushirikiano wa washikadau wengine wataendelea kuhusisha wawekezaji wa humu nchini na mataifa ya nje, serikali kuu, serikali za majimbo, na wadhibiti ili kuimarisha soko la hisa

**BWANA JOHN E. KIRIMI**
**MWENYEKITI WA KASIB**

**Taarifa kutoka kwa meneja mtendaji**

**UJUMBE WAKE MENEJA MTENDAJI WA SOKO LA HISA NA HATI ZA DHAMANA (NSE)**
Soko la NSE linaamini kwamba dunia huenda ikawa mahali bora zaidi iwapo kila mmoja atatumia kikamilifu uwezo aliyojaliwa kwa manufaa ya nafasi iliyopo.

Mwaka 2012, halmashauri ya wakurugenzi wa soko la hisa na hati za dhamana, NSE, iliidhinisha mpango wa kutoa mafunzo ya kifedha kwa wawekezaji kama mwongozo wa juhudi zake za kuwajibikia jamii.

Soko hili, linaamini kuwa wawekezaji wenye ufahamu wa habari mwafaka ndiyo walio bora dhidi ya kukabiliana na visa visivyohalali.
Kupitia kijitabu hiki cha kuelimisha wawekezaji, ni matumaini yetu kwamba hii ni njia moja ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya kifedha kwa wawekezaji kwenye soko letu.

Hata hivyo tunafuraha kushirikiana na chama cha madalali wa hisa na benki za uwekezaji nchini katika kuchapisha kijitabu hiki cha kuelimisha mwekezaji.

Tunaamini kwamba baada ya wewe kujifunza mengi kuhusu soko la hisa kupitia kijitabu hiki, utaweza kuelewa vyema soko la hisa. Kadhalika tunatumai utaweza kuvutiwa kuwekeza zaidi, kupanua shughuli zako za uwekezaji na kisha kujiimarisha kwa maisha.

**BWANA PETER MWANGI**
**MENEJA MTENDAJI WA NSE**

**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA INAYOTUMIKA KATIKA SOKO LA HISA:**
**MANENO MUHIMU**

**KASIB** – (*Kenya Association of Stockbrokers and Investment Banks*)
**Chama cha Kenya cha madalali wa hisa na benki za uwekezaji**
Ni chama kinachojumuisha kampuni za udalali wa hisa na benki za uwekezaji. Kina wanachama kumi na wanane na afisi zake ziko katikati mwa mji wa Nairobi katika jumba la city barabara ya standard.

**NSE** – *(Nairobi Securities Exchange)*
**Soko la hisa na hati za dhamana la Nairobi**
Soko la hisa na hati za dhamana ni soko lililotengwa katika sehemu moja kwa shughuli ya uuzaji na ununuzi wa hisa na hati za dhamana au pia ni soko linalotumia mfumo wa teknolojia wa kitarakilishi kushirikisha shughuli ya uuzaji na ununuzi wa hisa na hati za dhamana.
Nchini Kenya, soko la hisa na hati za dhamana ndilo soko pekee kwa sasa lililokubaliwa kuhudumu.

Soko hili lilianzishwa mwaka 1954

**CMA** – (*Capital Markets Authority)*

**Halmashauri ya masoko ya mtaji**

Ni halmashauri inayodhibiti sekta hii ya shughuli za hisa, hati za dhamana na hati nyinginezo zinazodumu kwa muda mrefu na ambazo zinauzwa au kunuliwa humu nchini. Halmashauri hii ilibuniwa kupitia sheria ya bunge ili kuimarisha, kudhibiti na kuhakikisha kuwa soko hili linastawi ipasavyo.

**Mfumo wa matumizi ya tarakilishi wa CDSC** – *(Central Depository And Settlement Corporation)*

Huu ni mfumo wa kutumia kompyuta kudhibiti akaunti ya mwekezaji ya CDS ambayo inahifadhi hisa au hati za dhamana alizonunua.

**Soko la hisa** – *(Stock Market)*

Hili ni soko ambalo ununuzi na uuzaji wa hisa unaendeshwa. Soko hili huziwezesha kampuni kupata mtaji huku wawekezaji wakipata umiliki wa kampuni, faida ya hatua hii hata hivyo, inategemea matokeo ya kibiashara ya kampuni.

Soko hili limegawanywa mara mbili; awamu ya kwanza inajumuisha toleo la kwanza la hisa za kampuni mbalimbali kwa umma na katika awamu ya pili toleo hili linauzwa katika soko la hisa la Nairobi.

**Hisa** – *(Stocks)*

Hisa ni umiliki wa sehemu ya kampuni. Hisa zinatolewa kwa umma na kampuni ili kupata mtaji na zinanunuliwa na wawekezaji ili kumiliki sehemu ya kampuni.

**Akaunti za hisa za CDS** – *(The Central Depository System)*

Hii ni akaunti ya hisa na inahudumu kama akaunti za benki ambapo mwekezaji anafungua akaunti yake na kuwekeza hisa zake kwenye akaunti hiyo kwa ajili ya kufanya biashara.

**Ajenti wa kusimamia akaunti za hisa** – *(A Central Depository Agent)*

Ajenti anaweza kuwa kampuni ya udalali au benki husika ambayo imeruhusiwa na CDSC kufungua, kufunga na kuhamisha akaunti kwa niaba ya mwekezaji.

## SEHEMU YA PILI:
## MANENO YANAYOTUMIKA KATIKA SOKO LA HISA

**Umiliki** *(Acquisition)*

Hali ambapo kampuni moja inachukua usimamizi wa kampuni nyingine kwa njia ya kirafiki au kwa kushindana.

**Hisa nyepesi /Rahisi** *(Active Share)*

Hizi ni hisa ambazo zinanunuliwa na kuuzwa katika soko la hisa kila mara. Hisa za kampuni maarufu huwa nyepesi.

**Ajenti** *(Agent)*

Huyu ni mwakilishi wa kampuni ya udalali au benki ya uwekezaji aliyeidhinishwa kufanya biashara ya ununuzi na uuzaji hisa kwa niaba ya kampuni husika.

**Agizo la ununuzi au uuzaji wa hisa zote au kutoshiriki** *(All or None {AON})*

Hili ni agizo linalotolewa kwa dalali kununua au kuuza hisa zote kufikia mwisho wa biashara za siku au kutoshiriki katika biashara hiyo.

**Kibali cha ugavi wa hisa** *(Allotment Letter)*

Hiki ni cheti kinachotolewa na kampuni kwa mwekezaji kudhihirisha thamani ya hisa alizogawiwa.

**Kuungana kwa kampuni** *(Amalgamation)*

Hatua hii hutokea ambapo kampuni mbili huru zinaungana pamoja na kuunda kampuni moja mpya.

**Ripoti ya kifedha ya kila mwaka** *(Annual Report)*
Ripoti ya kifedha inayotolewa na kampuni kwa wanahisa wake katika mwisho wa kipindi cha fedha. Ripoti hii inajumuisha ripoti za kifedha, oparesheni za kampuni, ukaguzi na habari nyinginezo kuhusu kampuni. Ripoti hii ni lazima itolewe na kampuni za umma.

**Mkutano mkuu wa kila mwaka** *(Annual General Meeting)*
Huu ni mkutano wa lazima unaoandaliwa na kampuni zote za umma kila mwaka. Wakati huo wakurugenzi wa kampuni wanatoa ripoti ya matokeo na mwelekeo wa kampuni siku zijazo kwa wanahisa. Wanahisa wote wanaalikwa na wanaruhusiwa kuuliza maswali. Ilani ya mkutano huo ni lazima izingatiwe.

**Cheti cha maelewano na kanuni za kampuni** *(Articles of Association)*
Hii ni stakabadhi inayoelezea umuhimu, mahali pa biashara na habari kuhusu kampuni. Kampuni zote husika zinahitajika kisheria kuwa na cheti hiki na kuwasilisha kwa msajili wa kampuni na kisha kufuata maagizo yake. Cheti hiki pamoja na kile cha mkataba wa maelewano vinaunda katiba ya kampuni.

**Muundo wa bei wa ASK** *(Ask)*
Hii ni bei ya chini ya hisa ambayo muuzaji anakubali na inaashiria idadi ya hisa angependa kuuza.

**Raslimali au mali** *(Assets)*
Hii ni mali inayomilikiwa na kampuni kama vile shamba, majengo, vifaa, pesa na kadhalika.

**Agizo la bei bora** *(At Best Order)*
Hili ni agizo linalotolewa na mteja kwa dalali kumruhusu kutumia maarifa yake kupata bei bora ya hisa.

**Hisa zilizoidhinishwa kuuzwa** *(Authorized Shares {Stock})*
Hizi ni jumla za hisa za kampuni zilizoidhinishwa kuuzwa kulingana na vyeti vya maelewano. Kiwango cha hisa kinaweza tu kuongezwa baada ya uamuzi kufanywa na idadi kubwa ya wanahisa na maombi kutumwa kwa msajili wa kampuni.

**Mtaji wa hisa ulioidhinishwa** *(Authorized Share Capital)*
Kiwango hiki ni cha mtaji wa hisa ulioidhinishwa na kujumuishwa katika vyeti vya maelewano.

**Biashara ya hisa kwa kutumia kompyuta** *(Automated Trading System {ATS})*
Mfumo wa ununuzi na uuzaji wa hisa kwa kutumia tarakilishi katika soko la hisa la Nairobi. Biashara ya hisa inaweza kuendelezwa katika sakafu ya soko la hisa au kwenye afisi za madalali. Mfumo huo unasimamiwa na soko la hisa la Nairobi.

**Kiwango kilicho chini ya wastani** *(Averaging Down)*
Ni kiwango kinachohusu ununuzi wa hisa nyingi kwa bei ya chini ikilinganishwa na bei ya awali ya uwekezaji ili kupunguza gharama ya kila hisa iliyonunuliwa.

***

**Afisi isiyotumika moja kwa moja na mwekezaji** *(Back Office)*
Hii ni sehemu ya afisi ya kampuni ya udalali isiyo na uhusiano wa moja kwa moja na wawekezaji na inahusika na shughuli karibu zote za soko.

**Shughuli yenye hitilafu** *(Bad Delivery)*
Hali hii hutokea iwapo cheti cha hisa na kile cha uhamisho havimfikii mwekezaji kwa muda unaopaswa. Hii hutokana na dosari katika majina na hitilafu nyinginezo. Iwapo dalali wako anakupa stakabadhi yenye hitilafu anatakiwa akutafutie nyingine sahihi na cheti cha uhamisho.

**Pointi ya msingi** *(Basic Point)*
Ni asilii mia moja ya alama, kwa mfano tofauti iliyopo kati ya asilimia 4.50 na 4.75 ni pointi 25 ya msingi.

**Dalali wa kutarajia faida kutokana na upungufu wa bei** *(Bear)*
Dalali anayebahatisha kupata faida kwa kutarajia kuwa bei ya hisa itapungua na kisha kuuza hisa zake kwa bei ya chini. Kila mwekezaji anaweza kujishughulisha na hali hii wakati mmoja na wengine kila mara.

**Kipindi cha upungufu wa bei ya hisa** *(Bear Market/Bear Cycle)*
Huu ni wakati ambapo muda wa kupungua kwa bei ya hisa unaongezeka na kiwango cha kampuni bora pia kinaendelea kushuka.

**Kengele** *(Bell)*
Kengele inayopigwa inaashiria ufunguzi na mwisho wa  shughuli za kibiashara kwa siku kwenye ukumbi au ssakafu ya soko la hisa na hati za dhamana. Kuna kengele ambayo hupigwa wakati wa kuanzisha biashara na kisha wakati wa kukamilisha biashara za siku mtawalia. Tangu kuanzishwa  kikamilifu  kwa matumizi ya kielektroniki  mwezi septemba, tarehe 22 mwaka 2006, kengele ilipigwa  kuashiria  matukio muhimu kama vile wakati wa kuorodheshwa na mwanzo wa biashara ya hisa mpya.

**Mmliki halali wa hisa** *(Beneficial Owner)*
Huyu ni mwekezaji halali anaye pokea faida hata ingawa anwani ya kibali ina jina tofauti.

**Zabuni** *(Bid)*
Hii ni bei ya juu zaidi inayowaniwa na mwekezaji. Hata hivyo inaashiria idadi ya hisa mwekezaji anahitaji kununua.

**Amri ya hisa nyingi** *(Block Order)*
Hii ni amri inayotolewa na mwekezaji kwa dalali ili kununua au kuuza idadi kubwa ya hisa.

**Hisa za kampuni maarufu** *(Blue Chip Stocks)*
Hizi ni hisa za kampuni zilizo na kiwango cha juu cha mtaji, ni maarufu na zinazojulikana nchini kwa mapato bora na pia zinalipa mgao bora wa faida kwa wanahisa wake.

**Hati za dhamana** *(Bonds)*
Hizi ni dhamana zinzodumu kwa muda mrefu. Zinauzwa na serikali na mashirika, huku faida ikipatikana baada ya kipindi fulani na jumla ya thamani ya uwekezaji huo ikilipwa baada ya kukamilika kwa kipindi chote cha uwekezaji.
Hati za dhamana hazina umiliki wowote ikilinganishwa
na hisa na kuna uhakika wa kupata riba hata wakati kampuni inaandikisha hasara.

**Toleo la pili la hati za dhamana** *(Bonus Issue)*
Hizi ni hati ziada za dhamana zinazotolewa kwa wanahisa kulingana na idadi ya hisa wanazomiliki na hakuna gharama yoyote inayoshuhudiwa.

**Kufungwa kwa orodha ya usajili** *(Book Closure)*
Huu ni wakati ambapo kampuni hutangaza kutolewa kwa mgao wa faida au hisa za bure kwa wanahisa wake.

**Hasara isiyoshuhudiwa na mwekezaji** (Book Loss)
Hii ni hasara inayotokana na kupungua kwa thamani ya hisa lakini haishuhudiwi na kuendelezwa kwani mwekezaji hajauza hisa wakati wa upungufu huo.

**Faida isiyoshuhudiwa na mwekezaji** *(Book Profit)*
Ni wakati ambapo thamani ya hisa inaimarika kwa kuongezeka kwa bei lakini faida hiyo haishuhudiwi moja kwa moja na mwekezaji kwani hajauza hisa zake.

**Bourse** *(Brouse)*
Jina hili pia lina maana sawa na soko la hisa na hati za dhamana

**Dalali** *(Broker)*
Huyu ni mwanachama wa soko la hisa la Nairobi aliyeidhinishwa kununuwa na kuuza hisa kwa niaba ya wawekezaji. Dalali hamiliki hisa za mwekezaji bali hulipa ada ya kuendesha biashara.

**Msubiri wa ongezeko la bei ili kupata faida** *(Bull)*
Huyu ni dalali anayetarajia bei ya hisa kuongezeka na hivyo basi hununua hisa ili kuuza baadaye na kupata faida.

***

**Faida kwa mtaji** *(Capital Gain)*
Faida kwa mtaji ni ongezeko katika thamani ya raslimali za mtaji. Faida zinapatikana tu baada ya kuuzwa kwa mali zinazomilikiwa.

**Hasara inayotokana na mtaji** *(Capital Loss)*
Hasara hii hutokana na kupungua kwa thamani ya raslimali za mtaji ukilinganisha na bei ya awali.

**Soko la mtaji** *(Capital Market)*
Ni mbinu ya kupata mtaji utakaodumu muda mrefu wa kustawisha kampuni. Soko la hisa ni sehemu ya soko la mtaji.

**Hifadhi za mtaji** *(Capital Reserves)*
Ni faida za kampuni ambazo hutolewa kama mgao wa faida kwa wanahisa. Hata hivyo zinaweza kutolewa kama hisa za bure.

**Mbinu za kupata mtaji** *(Capital Structure)*
Hii ni jinsi kampuni inavyofadhili oparesheni zake kwa kutumia mbinu tofauti tofauti kama vile mikopo ya muda mrefu na mfupi na utoaji hisa.

**Hati ya umiliki wa hisa** *(Certificate {Share Certificate})*
Stakabadhi inayothibitisha umiliki wa hisa, hati za dhamana au hati nyinginezo na mwekezaji. Hata hivyo baada ya kuanzishwa kwa mfumo wa biashara ya hisa kwa kutumia tarakilishi, utumizi wa stakabadhi za makaratasi ulifutiliwa mbali.

**Tarehe ya mwisho wa kutuma maombi** *(Closing Date of Offer)*
Hii ni tarehe ya mwisho inayokubaliwa kutuma maombi ya toleo la hisa/hati za dhamana.

**Bei ya kufunga biashara ya siku** *(Closing Price)*
Hii ni bei ya mwisho ya kufunga biashara za siku ambayo inapatikana baada ya kulinganishwa na ile ya hapo awali.

**Kanuni za maadili bora** *(Code of Ethics)*
Hii ni stakabadhi inayochapishwa na chama cha KASIB kama mwongozo wa udhibiti wa maadili baina ya wanachama wanaoendesha biashaara na wawekezaji.

**Uwekezaji wa jumla** *(Collective Investment Schemes)*
Uwekazaji huu unajumuisha ukusanyaji wa pesa kutoka kwa wawekezaji tofauti tofauti ambazo zinahifadhiwa kwa hazina moja na kusimamiwa na mtaalamu ambaye anawekeza kwa nafasi mbalimbali kulingana na lengo la hazina hiyo.

**Hazina maalum ya pamoja** *(Mutual Fund)*
Pesa zinakusanywa kutoka kwa wawekezaji wadogo na kuwekezwa kwenye hisa, hati za dhamana na hati nyinginezo kwenye hazina maalum.Kuna hazina ya maafikiano ya wazi ambayo inamruhusu mwekezaji mpya na pia inarejesha malipo ya uwekezaji wa wale wanaojiondoa. Hazina ya mfungo nayo ni imara na idadi fulani ya wawekezaji haibadiliki.

**Uwekezaji kwa kitengo maalum cha vipimo** *(Unit Trust)*
Uwekezaji wa pamoja kwa kukusanya pesa kutoka kwa wawekezaji wadogo na kutoa vipimo maalamu au 'units.' Mpango huu umeidhinishwa kupitia cheti cha uaminifu. Pesa zilizokusanywa zinawekezwa kwenye nafasi tofauti tofauti za uwekezaj na kudhibitiwa na mtaalamu wa maswala ya kifedha.

**Ushirikiano wa muda** *(Consortium)*
Huu ni ushirikiano wa muda kati ya kampuni mbili au zaidi kwa lengo la kupata mradi mkubwa. Kushirikiana katika maswala ya kifedha, kiufundi na wafanyikazi kunatoa ushindani bora dhidi ya kampuni nyingine zinazowania tenda au zabuni.

**Hisa zisizo za kawaida** *(Contarian Shares)*
Hizi ni hisa zinazo tofautiana na zile za kawaida ambapo zinaimarika wakati soko linapopungua.

**Umiliki wa hisa nyingi** *(Controlling Interest)*
Ni kumiliki idadi kubwa ya hisa za kampuni ili kusababisha mabadiliko ya sera. Umiliki wa hisa asilimia 50% na moja ziada unaweza kumpa mtu binafsi au kundi mamlaka ya kushawishi uamuzi wa kampuni.

**Bidhaa za uwekezaji zinazoweza kugeuzwa kwa urahisi** *(Convertible Security {Convertibles})*
Bidhaa hizi zinahusu hati za dhamana ambazo zinawezwa kubadilishwa na kuwa hisa za kawaida kulingana na maagizo.

**Udanganyifu kwa ripoti za kifedha** *(Cooking the Books)*
Hii ni kubadilisha ukweli halisi wa ripoti za kifedha kwa kujumuisha uwongo na kuifanya kampuni ionekane kwamba ina faida za juu ili kuwavutia wawekezaji.

**Mwongozo wa kampuni** *(Corporate Governance)*
Huu ni utaratibu unaozingatia shughuli, sheria na taasisi zinazotoa mwongozo wa udhibiti wa kampuni. Mwongozo huu unaelekeza jinsi ya kutekeleza ugavi wa majukumu kati ya wahusika mbalimbali hususan baina ya wasimamizi na wanahisa.

**Mpango wa huduma kwa jamii** *(Corporate Social Responsibility {CSR})*
Ni kujitolea kwa kampuni ili kuendeleza maadili bora, kuchangia kwa ustawi wa uchumi na kuzingatia maslahi ya wafanyikazi na familia zao huku mazingira bora kwa jamii yakitiliwa mkazo.

**Shirika/Kampuni** *(Corporation/Company)*
Mtindo wa kibiashara uliyobuniwa chini ya sheria za Kampuni za Kenya ambao unafahamika kisheria na unatofautiana na wamiliki wake. Wamiliki wa shirika ni wanahisa na wanapaswa kulipa madeni ya kampuni yasiozidi kiwango chao cha uwekezaji.

**Kupungua na kuhakiki soko** *(Correction)*
Ni lugha inayotumika kueleza kupungua kwa soko kwa mfulilizo. Hata hivyo inasemekana kwamba soko halipaswi kuchukua mtindo wa kuimarika au kupungua kwa mfululizo kwani litahitajika kusahihishwa.

**Kuponi** *(Coupon)*
Hiki ni kiwango cha riba kinachopatikana kwa mapato yanayotokana na hisa au dhamana zilizouzwa. Hii pia ni riba kamili ya hati za dhamana za serikali ambayo hulipwa mara mbili kwa mwaka.

**Upungufu wa kima cha juu** *(Crash)*
Huku ni kupunguka zaidi kwa bei ya hisa katika kipindi kifupi.

**Uwezo wa kampuni wa kulipia mkopo** *(Credit Rating)*
Hii hutumika katika ukaguzi wa uthabiti wa kampuni au taasisi ya kifedha ili kupewa mkopo. Hatua hii hutekelezwa ili kufahamisha wawekezaji hatari iliyopo.

**Kuorodheshwa kwa masoko tofauti** *(Cross Listing)*
Hii ni wakati kampuni inapoorodhesha hisa zake katika masoko tofauti tofauti mbali na soko lake tangulizi.

**Hisa zenye mgao wa faida** (Cum Dividend)
Mmiliki wa hisa zenye mgao wa faida anaruhusiwa kupokea mgao uliopendekezwa na kuidhinishwa.

**Hisa zenye haki miliki** *(Cum Rights)*
Mnunuzi wa hisa hizi anaruhusiwa kushiriki katika utoaji wa hisa ziada za haki miliki zilizotangazwa na kampuni.

**Taasisi simamizi ya kifedha** *(Custodian)*
Hii ni taasisi ya kifedha yenye majukumu ya kisheria na mamlaka ya kulinda vyema raslimali za mteja.

**Hisa zisizothabiti** *(Cyclical Share {Stock})*

Hisa hizi zinaathirika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi.
Bei ya hisa hizi huathiriwa na hali ya uchumi wa kitaifa na kimataifa, kwa mfano shughili za kitalii na kadhalika.

***

**Mkopo** *(Debentures)*
Huu ni mkopo wa muda mrefu unaochukuliwa na kampuni kwa kiwango fulani cha riba na pia unaweza kuchukuliwa dhidi ya rasli mali nyinginezo. Kuna mikopo iliyo na uwezo wa kubadilishwa kuwa hisa za kawaida baada ya kipindi fulani.

**Siku ya malipo ya mgao wa faida** *(Declaration Date)*
Ni siku inayotangazwa kuhusu ulipaji wa mgao wa faida katika kipindi kijacho. Hutangazwa na bodi ya wakurugenzi ya kampuni iliyoorodheshwa katika soko la hisa.

**Kupungua kwa bei ya hisa kwa kipindi fulani** *(Decline)*
Huu ni wakati ambapo bei ya hisa inapopungua katika siku Fulani ya mauzo na kufunga kwa bei ya chini ikilinganishwa na ile iliyofungua biashara za siku.

**Hisa thabiti** *(Defensive Stock)*
Hizi ni hisa za kampuni ambazo ni thabiti na mapato yake pamoja na malipo ya mgao wa faida yanabakia thabiti licha ya kipindi kigumu cha uchumi. Hupungua kwa kadri wakati soko linapopungua na mwekezaji hurejelea uwekezaji wake kama kawaida.

**Kutoorodheshwa kwa kampuni** *(Delisting)*
Ni wakati ambapo jina la kampuni linapoondolewa katika orodha rasmi ya soko la hisa na kukosa kushiriki katika biashara. Hali hii inatokana na kutofuata maagizo ya soko.

**Hisa au dhamana zisizotambulika kupitia hati za makaratasi** *(Dematerialzied Secutities)*
Hisa au hati hizi za dhamana zimefunguliwa akaunti za CDS na zinauzwa au kununuliwa kwa kutumia tarakilishi na stakabadhi zake za makaratasi hazitambuliki tena.

**Thamani kutoka kwa raslimali** *(Derivative)*
Ni mbinu ya kupata thamani kwa raslimali zilizopo kama vile hisa, sarafu, hati za dhamana na bidhaa nyinginezo.

**Kupungua kwa thamani ya hisa** *(Dilution of Equity)*
Hali hii inahusu upungufu wa thamani ya umiliki wa hisa kutokana na kuongezeka kwa hisa. Hatua hii husababisha upungufu wa thamani ya mapato kwa kila hisa.

**Kupunguza turuhani/Bei nafuu au ya chini** *(Discount)*
Tofauti ya kiwango cha chini iliyopo kati ya bei halisi ya hati za dhamana na bei ya sasa katika soko.

**Akaunti ya dalali** *(Discretionary Account)*
Hii ni akaunti inayofunguliwa na mwekezaji kwa ushirikiano wa dalali ambayo inampa mamlaka dalali kununua au kuuza hisa, hati za dhamana kwa uamuzi wake mwenyewe kwa niaba ya mwekezaji.

**Kupanua uwekezaji** *(Diversification)*
Ni mbinu ya kudhibiti hatari kwa kununua bidhaa tofauti tofauti za uwekezaji katika kampuni mbalimbali zinazowakilisha sekta za uchumi.

**Mgao wa faida** *(Dividend)*
Kiwango cha faida ya kampuni iliyoorodheshwa, kinacholipwa wenye hisa, kiwango hiki kinaamuliwa na bodi ya wakurugenzi na kuidhinishwa wakati wa mkutano mkuu wa kila maka. Kampuni iliyoorodheshwa haishurutishwi kulipa mgao wa faida.

**Mgao wa faida kwa kiwango cha silimia** *(Dividend Yield)*
Huu ni mgao wa faida ambao unawakilishwa kwa asilimia (%).

**Kiwango cha ununuzi wa hisa** *(Dollar Cost Averaging)*
Kuwekeza kiasi fulani cha pesa kwa aina yoyote ya uwekezaji katika kipindi kilichokusudiwa. Mwekezaji hununua hisa nyingi wakati bei imeshuka na chache wakati bei imepanda.

**Uwekezaji usiothibitika** *(Dry Run Portfolio)*
Uwekezaji huu pia unafahamika kuwa uwekezaji wa karatasi. Mwekezaji anachunguza na kusjiriki biashara ya ununuzi na uuzajii wa hisa kupitia mawazo yake.
Mwekezaji wa aina hii anapata tajriba kuhusu changamoto na faida zinazotokana na soko bila ya kushuhudia gharama yoyote huku imani katika biashara hii inaimarika na anaweza kuamua kushiriki.

***

**Faida halisi ya mapato ya hisa** *(Earnings per Share)*
Hii ni faida ya kampuni baada ya kutozwa ushuru ambayo inatengewa kila hisa za kawaida.
Ni ishara ya kupatikana kwa faida ya kampuni na inatumika kupata bei halisi ya hisa.

**Mapato ya kampuni** *(Earnings Yield)*
Hii ni tofauti iliyopo baada ya kutenga faida halisi ya kampuni na jumla ya thamani ya hisa kwa bei ya soko.

**Hisa za lazima** *(Eating Stock)*
Hizi ni hisa au hati za dhamana ambapo mwekezaji analazimika kununua bila ya kuvutiwa

**Amana za kupata mkopo (*Eligible Securities)***
Hizi ni hisa, mikopo spesheli na hati za dhamana zinazokubaliwa na benki kusimamia mkopo. Idadi kubwa ya hisa katika soko la hisa la Nairobi hukubalika kama amana za kupata mkopo.

**Mpango wa umiliki wa hisa** *(Employees Share Ownership Plan {ESOP})*
Huu ni mpango unaohakikisha kuwa hisa zinagawiwa wafanyikazi wa kampuni ili kuwavutia kufanya kazi kwa bidii kama wanahisa wa kampuni hiyo.

**Hisa zilizomilikiwa kwa pamoja** *(Encumbered Securities)*
Hisa hizi humilikiwa na mtu au kundi lakini mtu mwingine au kundi lingine linaweza kuingilia kati ili kupata umiliki. Hii hutokea wakati hisa au dhamana zimetumika katika kupokea mkopo.

**Uuzaji wa hisa ili kupata mtaji** *(Equity Financing)*
Kampuni inauza hisa zake ili kukusanya mtaji. Wanunuzi wanakuwa wamiliki wa kampuni na wanapata riba.

**Soko la hisa** *(Equity Market)*
Hili ni soko ambalo hisa zinauzwa na kununuliwa kupitia sehemu maalum au katika maeneo rejareja (OTC) yanayoendeshwa na madalali pamoja na wahusika wengine.
Soko hili ni muhimu kwa uchumi kwani hutoa nafasi kwa kampuni kukusanya mtaji na kutoa nafasi kwa wawekezaji kumiliki kampuni hizo kadri ya hisa walizonunua.
Soko hili limegawanywa mara mbili. Kuna soko la utangulizi ambapo hisa mpya zinatolewa kwa umma kwa mara ya kwanza na soko la upili au sekondari ambapo hisa zilizotolewa katika soko la utangulizi zinauzwa katika soko la hisa la Nairobi.

**Jumla ya thamani ya hisa** *(Equity Market Capitalization)*
Ni kiwango kamili cha thamani ya hisa na kinajumuisha thamani ya hisa zote za kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa. Hutumika kupima ongezeko au upungufu wa soko.

**Wanahisa wa kawaida** *(Equity Shareholders)*
Hawa ni wamiliki wa hisa na wanashiriki katika faida au hasara inayoshuhudiwa na kampuni. Wanaruhusiwa kupiga kura wakati wa mikutano ya kampuni.

**Maadili ya uwekezaji** *(Ethical Investing)*
Huu uwekezaji unaongozwa na maadili ya mwekezaji na si mahitaji ya kifedha. Mwekezaji anaweza kuwekeza kwa kiwango cha juu katika kampuni zinazoambatana na maadili yake na si kampuni nyingine kama vile za pombe, n.k.

**Bila mgao wa faida** ***(Ex Dividend)***
Mmiliki wa hisa aina hizi hawezi kupata mgao wa faida ufuatao lakini anaweza kupata mgao wa siku za usoni.

**Ukosefu wa hisa za haki miliki** ***(Ex Right)***
Anayemiliki hisa hizi hatapokea hisa miliki zilizopendekezwa sasa hadi hapo baadaye.

**Ubadilishanaji (Exchange)**
ona **Stock Exchange**

**Mgao wa faida spesheli** ***(Extra Dividend)***
Mgao wa faida wa ziada unaongezewa mwekezaji.

**Mkutano maalum** ***(Extraordinary General Meeting)***
Huu ni mkutano wowote spesheli mbali na ule mkuu wa kila mwaka ambao unaitishwa ili wanahisa waidhinishe maswala ya dharura. Maswala haya yanaweza kuwa kuondolewa kwa mkurugenzi mkuu, kununuliwa kwa kampuni, kuungana na nyingine, n.k.

***

**Kiwango kamili cha gharama ya mkopo** ***(Face Value)***
Hiki ni kiwango halisi cha jumla ya gharama ya hati za dhamana baada ya kukamilika kwa muda uliowekwa.

**Taasisi ya kifedha** ***(Financial Institution)***
Hii ni kampuni au mashirika yanayosimamia maswala ya kifedha. Kwa mfano kuna benki inayokusanya fedha za akiba kutoka kwa wawekezaji na kisha inakopesha wanaohitaji mkopo. Baadhi ya taasisi hizi zina kiwango kikubwa cha fedha na zinauwezo mkubwa wa kuathiri bei za bidhaa za kifedha katika soko la hisa.

**Bidhaa za kifedha** ***(Financial Instrument)***
Hii inahusu kandarasi inayowakilisha maelewano yenye thamani ya fedha. Aidha bidhaa za kifedha zinajumuisha umiliki wa mali zinazotokana na hisa,au makubaliano ya mkopo uliochukuliwa na mwekezaji kupitia umiliki wa hisa na hati. Kadhalika, kuna bidhaa zingine za kigeni za ubadilishanaji wa fedha.

**Masoko ya kifedha** ***(Financial Markets)***
Haya ni masoko ambapo wanunuzi na wauzaji wa bidhaa za kifedha kama vile hisa, hati za dhamana, sarafu na bidhaa zinazotokana na thamani ya hisa au bidhaa zinginezo( derivatives)hukutana.
Masoko hayo yanajumuisha masoko ya kifedha na mtaji.

**Mtindo wa kuepuka athari za uwekezaji** ***(Financial Pyramid)***
Hii ni mbinu inayotumika na wawekezaji ambao wangependa kuwekeza kwa nafasi tofauti tofauti kwa misingi ya usalama na faida. Kwa mfano, uwekezaji kwa dhamana za serikali ambazo zina faida kubwa na bidhaa nyinginezo.

**Mwaka wa kifedha** ***(Fiscal Year)***
Ni kipindi cha miezi 12 ambacho kampuni hutumia kwa madhumuni ya uhasibu wa matokeo yake. Kipindi hiki kinaweza kukosa kuwiana na kalenda ya kawaida ya kila mwaka au kipindi cha fedha cha serikali.

**Raslimali zinazodumu kwa muda mrefu** ***(Fixed Assets)***
Rasilmali hizi zinajumuisha mashamba, majengo, mashine, viwanda na vitu ambavyo havikusudiwi kubadilishwa kuwa pesa taslimu kwa urahisi.

**Uwekezaji wenye mapato ya muda mrefu** ***(Fixed Income Investments)***
Ni uwekazaji katika akiba, mikopo isiyogeuzwa kuwa hisa, hati za dhamana za serikali na huchangia riba iliyothabiti.

**Bei isiyoyumba yumba kwa muda** ***(Flat)***
Hii ni bei isiyopungua wala kuongezeka kwa mfano hisa za kampuni zinaweza kusalia kwa bei ya shilingi 12 katika muda wa mwezi mmoja uliopita.

**Hazina nyepesi au afua** *(Flexible Fund)*
Hazina hii inaweza kubadilisha mkakati wake wa uwekezaji na kuwekeza pesa zilizokusanywa katika bidhaa tofauti tofauti zinazoaminika kuwa bora ili kuimarisha mapatao badala ya kuangazia uwekezaji wa bidhaa moja pekee.

**Jumla ya hisa zilizotolewa katika mauzo** *(Float)*
Hisa hizi hutolewa na kampuni iliyoorodheshwa na inayomilikiwa na uma ili kuuzwa kwa soko la hisa.

**Biashara haramu** *(Front Running)*
Shughuli hii si halali kwani dalali ananunua na kuuza hisa kwa jina lake akisubiri amri kutoka kwa mwekezaji.

**Mtaalam wa kifedha** *(Fund Manager)*
Ni mtu mwenye ufahamu wa maswala ya kifedha ambaye anasimamia hazina inayajumuisha hisa, hati za dhamana kwa niaba ya mwekezaji.

**Mkataba kuhusu biashara ya usoni** *(Futures Contract)*
Huu mkataba unahusu ununuzi au uuzaji wa hisa, dhamana na sarafu kwa bei fulani katika kipindi kilichoafikiwa katika siku zijazo. Hii ni biashara itakayotelekezwa hapo mbeleni.

***

**Ubinafsishwaji** *(Going Private)*
Kampuni hubadilisha umiliki wake kwa kubinafsishwa kupitia uuzaji tena wa hisa zake zote au kununuliwa na mtu binafsi. Hii hutokea wakati ambapo hisa za kampuni zina bei ya chini, au inahitaji kufanyiwa ukarabati.

**Kuuza hisa kwa umma** *(Going Public)*
Kampuni huuza hisa zake kwa umma kupitia toleo la kwanza ili kupata mtaji wa kufadhili mipango yake ya ustawi.

**Kuandikisha upungufu** (Going Short)
ona **Short Selling - Short Sale**

**Uhamisho bora wa hisa** *(Good Delivery)*
Huu ni wakati ambapo cheti cha umiliki na uhamisho wa hisa vinaambatana na maagizo ya uhamisho. Vyeti hivi vinamfikia mwekezaji kwa muda unaostahili na havina hitilafu.

**Hati za dhamana za serikali** *(Govenment Paper)*
Hutolewa au kusimamiwa na serikali.

**Hisa za kuandikisha ukuaji na kuwekezwa kwa muda** *(Growth Shares)*
Hizi hisa zinazoandikisha ukuaji wa juu sana kulingana na kiwango cha wastani cha mapato ya hisa na soko kwa jumla. Hisa hizi zinatarajiwa kuendelea na mkondo huo na ni bora za kuwekeza kwa muda mrefu.

**Udhamini wa hati za dhamana** *(Guaranteed Bond)*
Riba na kiwango cha pesa za uwekezaji zinadhaminiwa aidha na kampuni kuu au taasisi nyingine maarufu.

**Udhamini wa hisa** *(Guaranteed Stock {Shares})*
Hizi ni hisa ambazo mgao wake wa faida unadhaminiwa na kampuni nyingine. Kutokana na udhamini huo wawekezaji wako tayari kununua hisa nyingi.

**Biashara haramu inayohusu utumizi wa habari za siri** *(Gun Jumping)*
Biashara haramu ya ununuzi na uuzaji wa hisa za kampuni kwa kutumia habari za ndani ya kampuni kabla ya hisa hizo kutolewa kwa umma.

***

**Mbinu ya uwekezaji ya kukwepa hatari** *(Hedge)*

Hii ni mbinu inayotumika kupunguza hatari au hasara inayosababishwa na kupungua au kuongezeka zaidi kwa bei ya hisa na hati za dhamana kwa kuwekeza kwenye hisa au hati zilizo na uhusiano wa karibu. Wawekezaji hutumia mbinu hii wanapokosa uhakika jinsi soko linavyoendelea.

**Kuepuka athari za mfumko wa bei kwa kuzingatia bidhaa m badala** ***(Hedging Against Infalation)***
Hii ni mbinu hutumika kulinda raslimali za mwekezaji dhidi ya hasara inayosababishwa na mfumuko wa bei kwa kuweka kwa bidha zitakazopanda bei kama vile hisa za kawaida.

**Bei ya juu ya hisa** ***(High)***
Hii ni bei ya juu zaidi iliyolipwa kwa kununua au kuuza hisa wakati mmoja wa mauzo na mara kwa mara si sawa na ile ya kufunga biashara ya siku.

**Mbinu ya kuimarisha umaarufu wa hisa hafifu** ***(High Close)***
Mbinu inayotumiwa kwa hisa zisizo maarufu wakati wa dakika za mwisho za kufunga biashara ambapo maombi ya kiwango kidogo cha hisa hizo kwa bei ya juu yanaongezwa ili kuonekakana kuwa maarufu. Hata hivyo hali si hivyo kwani bei ya kufunga biashara za siku ndiyo uzingatiwa na kumvutia mwekezaji.

**Kiwango cha kihistoria cha kuyumbayumba kwa hisa** **(Historical volatility {HV})**
Hiki ni kiwango kinachotokana na kuyumbayumba kwa bei ya hisa kwa kipindi fulani. Kiwango hiki kinaathirika na mabadiliko katika soko.

**Mmiliki halali wa stakabadhi za hisa** ***(Holder of Record)***
Mtu au kampuni iliyosajiliwa kwa jina linalofahamika kumiliki hisa na anaruhusiwa kulipwa mgao wa faida au riba.

**Kampuni yenye kiwango cha juu cha hisa** ***(Holding Company)***
Ni kampuni ambayo si lazima ipate asilimia 51 ya hisa bali ifikishe hisa zinazotosha kushawishi uamuzi kama vile kusimamia oparasheni na kuchagua bodi ya wasimamizi.

**Toleo la kwanza lenye umaarufu** ***(Hot Issue)***
Hili ni toleo la kwanza linalovutia idadi kubwa ya maombi. Maombi yake huzidi kile kiwango kilichotarajiwa kama vile toleo la safaricom la mwaka 2008.

**Maagizo au sera za ndani za madalali** ***(House Rules)***
Hizi ni sera za ndani za kutoa mwongozo kwa madalali pamoja na utaratibu unaopaswa kufuatwa katika kushughulika na akaunti za wateja. Sera hizi zinanuia kuhakikisha kwamba madalali wanazingatia maagizo yaliyoidhinishwa. Masharti hayo yanatoa adhabu kali ikilinganishwa na masharti ya nje.

**Soko lenye uhuru wa matumizi ya kieletroniki au mtindo wa kale** ***(Hybrid Market)***
Soko hili linaruhusu uuzaji na ununuzi kufanyika kupitia mfumo wa kielektroniki au kwenye sakafu ya sehemu ya soko la hisa la Nairobi.

**Umiliki wa mali za walioshindwa kulipa madeni** ***(Hypothecation)***
Jina hili hutumika mara mbili. Kwanza kabisa hii inahusu mdalali wa hisa anapokubali kutumia hisa za mwekezaji kama dhamana kwa mkopo wa kununua hisa zaidi au pia mkopeshaji anapochukua mali za mtu aliyeshindwa kulipa mkopo kulingana na masharti yaliyopo.

***

**Agizo la kusimamisha biashara kwa muda** ***(Imbalance of Orders)***
Hutokea ambapo mnunuzi anapotuma maombi mengi ya ununuzi wa hisa kupita maombi ya uuzaji. Hii husababisha kusimamishwa kwa mauzo kwa muda na kuchelewesha biashara ya siku.
Hali hii ya ununuzi na uuzaji huchochewa na habari njema au habari za kusikitisha.

**Kufutiliwa mbali kwa matumizi ya karatasi** ***(Immobilization)***
Matumizi ya stakabadhi za makaratasi hayahitajiki kamwe na habari muhimu zilizohifadhiwa katika makaratasi haya zimejumuishwa kwenye tarakilishi na kusimamiwa na mfumo wa CDSC.

**Hisa zinazochukuwa kipindi kirefu kushuhudia biashara** *(Inactive Stock)*
Hisa hizi hazinunuliwi au kuuzwa mara kwa mara katika soko la hisa au lile soko la wazi.

**Hisa za mapato bora** *(Income Stock)*
Hisa hizi zinaendeleza malipo bora ya mgao wa faida na mgao huo ni wa kiwango cha juu ikilinganishwa na malipo ya soko la hisa.

**Kandarasi kati ya mnunuzi na muuzaji wa dhamana** *(Indenture)*
Mkataba huu unahusu malipo ya viwango vya riba kutokana na ununuzi wa hati za dhamana na pia unaelezea majukumu baina ya wahusika.

**Kipimo cha soko** *(Index)*
Kiwango hiki kinaangazia matokeo ya hisa. Kiwango hiki kinaundwa kutumia mbinu tofautitofauti katika masoko ya ulimwengu na kinawakilisha soko la hisa kwa jumla.

**Alama ya Kampuni bora 20** *(NSE 20 Share Index)*
Kiwago hiki kinaaagazia kampuni ishirini bora zilizoorodheshwa katika soko la hisa la Nairobi.

**Tazama Apex 2**
**Kiwango cha NASI (The NSE 20 Share Index)**
Kiwango hiki kinajumuisha hisa zote zilizoorodheshwa.

**Kupima ustawi wa soko** *(The NSE All Share Index (Nasi)*
Mkakati wa uwekezaji ambapo unachunguza jinsi kiwango cha hisa kinavyoimarika au kupungua.

**Kipimo cha Kampuni 27 kulingana na AIG (AIG 27 Index)**
Kiwango kinacho jumuisha kampuni 27

**Alama au kipimo maalum cha kiwango cha hisa** *(Indexing)*
Huu ni mkakati wa uwekezaji ambapo kundi la hisa tofautitofauti linaundwa ili kutoa picha halisi ya matokeo ya alama ya hisa zinazojumuishwa.

**Dalili za mgao sawa wa faida** *(Indicated Divided)*
Hii ni ishara ya kulipwa mgao sawa wa faida katika kipindi chote cha kifedha.

**Toleo la kwanza la hisa** *(Initial Public Offering {IPO})*
Hili ni toleo la mara ya kwanza la hisa za kampuni ya kibinafsi kwa uma. Hutekelezwa kupitia soko la hisa na huvutia kiasi kikubwa cha mtaji.

**Habari za ndani kuhusu Kampuni** *(Inside Information)*
Habari hizi ni nyeti na zinafahamika tu kwa wakurugenzi wa bodi, wasimamizi na wafanyikazi wa kampuni na si watu wa nje. Habari hizi zikitoka nje zitaathiri bei ya hisa za kampuni.

**Walio na ruhusa ya kupata habari za ndani** *(Insider)*
Ni watu ambao wana habari muhimu kuhusu kampuni na habari hizo hazijulikani kwa umma. Kama vile upanuzi, matokeo ya fedha na kadhalika. Watu hawa wanaweza kuwa wasimamizi, dalali, familia na marafiki.

**Biashara inayoegemea habari za kampuni** *(Insider Trading)*
Hutokea ambapo wale walio ndani wanatekeleza biashara kutumia habari iliyopo na haijulikani kwa umma. Hatua hii si halali kwa sababu wakati mwingine walio ndani ya kampuni wanunua hisa bila ya umma kufahamu huku wakikosa kufaidika.

**Mashirika ya uwekezaji** *(Institutional Investor)*
Mwekezaji huyu anawekeza idadi kubwa ya hisa na hati za dhamana. Mashirika haya yanajumuisha hazina ya Mutual Trust, Kampuni za Bima n.k.

**Riba** *(Interest)*
Ada inayotozwa kwa kukopa pesa na pia ni faida ya umiliki wa hisa.

**Riba (Interest)**
Kiwango cha pesa kinachomilikiwa na mwanahisa kwenye kampuni  na mara kwa mara huandikishwa kwa alama ya asilimia. Pia humaanisha malipo ya kuwekeza kwenye hisa au riba kwa mkopo.

**Mmiliki wa hisa za juu** ***(Interested Shareholder)***
Mwanahisa huyu anauwezo wa kushawishi uamuzi na sera ya kampuni.

**Mgao wa faida wa muda** ***(Interim Dividend)***
Huu ni mgao wa faida unaopendekezwa na kulipwa kabla ya kuandaliwa kwa mkutano mkuu wa kila mwaka na ripoti za kifedha.

**Mauzo ya siku** ***(Intraday)***
Inatumika kuonyesha jinsi bei ya hisa ilivyobadilika kwa siku katika kikao kimoja cha kibiashara. Kwa mfano , hisa inapofikia kiwango hicho ina maana kwamba inauza kwa bei mpya na ya juu ikilinganishwa na bei nyinginezo zilizoandikishwa siku hiyo.

**Mshauri wa uwekezaji** ***(Investment Advisor)***
Ni mtu au shirika lililoajiriwa na taasisi za kifedha au mtu binafsi kutoa ushauri kuhusu uwekezaji na jinsi ya kusimamia vyema raslimali.

**Benki ya uwekezaji** ***(Investment Bank)***
Hii ni taasisi inayotafutia mtaji kampuni zingine. Benki hii hutoa ushauri na ni ajenti katika toleo la kwanza la hisa. Benki hii pia hutoa huduma za udalali wa hisa na inaweza kufanya biashara katika soko la hisa kwa kutumia akaunti zake.

**Mazingira ya uwekezaji** ***(Investment Climate)***
Hii inahusu hali ya kiuchumi ya wawekezaji na huathiriwa na maswala ya kisiasa na kijamii. kwa mfano iwapo kuna hali ya sintofahamu katika siasa wawekezaji huogopa kuwekeza katika soko la  mtaji.

**Kilabu cha uwekezaji** ***(Investment Club)***
Hiki ni chama huru cha watu wanaokusanya pesa kuwekeza kwa pamoja wakati uwekezaji wa mtu binafsi hautoshelezi. Uwekezaji huu una kiwango cha chini cha hatari na hufaidi sana wawekezaji wadogo.

**Kampuni ya uwekezaji** ***(Investment Company)***
Kampuni hii huwekeza pesa zilizokusanywa kati ya makundi ya wawekekezaji warejareja kwa kununua na kuuza hisa. Kampuni hii huwawezesha wawekezaji wadogo kufikia bidha mbali mbali za uwekezaji. Kuna kampuni zilizowazi ambazo zinaendelea kupokea wawekezaji na pia kuna zile ambazo zina idadi fulani ya wawekezaji na hazibadili msimo wake.

**Muda unaopaswa kati ya ununuzi na uuzaji wa hisa** ***(Investment Horizon)***
Jumla ya muda uliyopo kati ya ununuzi na uzaji wa hisa ambao umepangwa na mwekezaji. Unaweza kudumu kwa miaka, miezi, majuma na hata siku.

**Mwekezaji** ***(Investor)***
Ni mtu binafsi au taasisi ambazo hutoa pesa ili kununua hisa au hati za dhamana kwa kutarajia faida.

**Hazina ya kutoa fidia kwa wawekezaji** ***(Investor Compensation Fund)***
Ni hazina speshali iliyotengwa kuwafidia wawekezaji katika soko la hisa wanapopata hasara kutokana na kufilisika kwa kampuni ya udalali au kutowajibikia wawekezaji ipasavyo.

**Toleo la hisa au hati za dhamana** ***(Issue)***
Hizi ni hisa au hati za dhamana ambazo zimetolewa na shirika au serikali kuuzia umma.

**Bei ya toleo** ***(Issue Price)***
Bei ya kwanza ya toleo la hisa kwa umma. Bei hii huamuliwa kwa ushirikiano na kampuni iliyoteuliwa kutoa ushauri  hususan benki ya uwekezaji.

**Hisa zilizotolewa kwa umma** *(Issued Shares)*
Idadi ya hisa za kampuni ambazo zimeuziwa wanahisa na si lazima kampuni iuze jumla ya hisa zilizoidhinishwa.

**Kampuni inayouzia umma umiliki** *(Issuer)*
Inaweza kuwa kampuni nyingine au serikali inayouzia umma hisa hati za dhamana ili kufadhili oparesheni zake.

***

**Dhamana ya wafadhili wengi** *(Joint Bond)*
Hati hii ya dhamana inafadhiliwa na wadhamini wawili au zaidi akiwemo mshiriki mkuu aliyeuzia umma hati hiyo. Mali za wafadhili zinatumika kulipa wanunuzi wa hati hiyo iwapo kuna hitilafu ya kifedha. Mara kwa mara kampuni kuu hufadhili mkopo uliochukuliwa na kampuni tanzu.

**Ushirikiano wa wanunuzi** *(Joint Holders)*
Ni wakati ambapo watu wawili au zaidi wanajiunga pamoja kununua hisa au hati za dhamana na wanazimiliki kwa pamoja. Washiriki wote wanapaswa kutia sahihi cheti cha uhamisho wa hisa.

***

**Kipimo cha ustawi wa kampuni** *(Key Performance Indicators)*
Ni mbinu tofautitofauti zinazotumika na kampuni mbalimbali kupima jinsi hali ya biashara ilivyo. Mbinu hizi zinaweza kuwa za kifedha au zenye mtindo tofauti.

**Kufahamu vyema mteja wako** *(Know Your Customer {KYC})*
Ni lazima dalali afahamu vyema mahitaji ya kifedha na maswala mengine ya mwekezaji kabla ya kufanya mapendekezo yoyote.
Hii itamwezesha kujua vyema bidhaa za uwekezaji zinazo mfaa mteja.

***

**Kampuni zenye mtaji wa juu** *(Large Cap)*
Thamani ya mtaji wa kampuni hizi ni wenye kiwango kikubwa katika soko.

**Siku ya mwisho ya usajili** *(Last Day to Register)*
Hii ni siku ya mwisho inayohitaji hisa au hati za dhamana kusajiliwa katika afisi ya muuzaji ili kufaidika kutokana na mgao wa faida, hisa ziada na hisa za haki miliki.

**Masharti yanayoambatana na mikopo** *(Lien)*
Masharti haya yanatolewa na benki au mkopeshaji hadi mkopo uliochukuliwa utakapolipwa. La sivyo raslimali za mwekezaji kama vile hisa zitasalia kushikilia nafsi ya mkopo kama.

**Agizo la ununuzi au uuzaji wa kiwango fulani cha hisa** *(Limit Order)*
Agizo hili linatolewa na mwekezaji pamoja na dalali kununua idadi fulani ya hisa kwa bei ya chini au kuuza hisa kwa bei ya juu. Agizo hili linatolewa ili mwekezaji asilipe bei ya juu iklinganishwa na ile waliokubaliana na dalali.

**Kufilisika kwa kampuni** *(Liquidation)*
Kufunga kwa kampuni kufatia matatizo ya kifedha au uamuzi wa wanahisa. Mali za kampuni huuzwa na faida inayosalia hutolewa kwa wanahisa.

**Raslimali nyepesi kwa kubadilisha kuwa pesa.** *(Liquidity)*
Raslimali hizi ni kama vile hisa ambazo zinaweza kununuliwa au kuuzwa kwa haraka bila ya kusababisha mabadiliko makubwa katika bei ya hisa. Raslimali hizi pia zinaweza kubadilishwa haraka ili kuleta pesa taslimu

**Kampuni za hisa zilizoorodheshwa katika soko la hisa** *(Listed Shares/Listed Company)*
Hisa hizi zimeorodheshwa kwenye soko la hisa linalofahamika ili kuuzwa. Hisa hizi zinaweza kuoorodheshwa kwa masoko mengine.

**Marsharti yakuorodheshwa** ***(Listing Requirements)***
Masharti haya yanatolewa na soko la hisa kwa kampuni ambazo zingependa kuorodheshwa katika soko hili. Ni sharti kampuni zifuate maagizo haya ili kuendeleza biashara zake katika soko la hisa. Masharti haya yanajumuisha idadi ya hisa, mtaji na mapato ya kampuni.

**Soko lenye ushindani mkali** ***(Locked Market)***
Soko hili lina hisa zenye bei sawa.

**Kushikilia hisa kwa muda mrefu (*Long position)***
Ni hali ya kuashiria umiliki wa hisa kwa matarajio kwamba thamani yake itaimarika . Jina hili pia hutumika kwa mtu anayemiliki hisa kwenye kampuni.

**Nafasi ndefu na finyu katika uuzaji wa hisa** ***(Long Squeeze)***
Hali hii hutokea wakati ambapo thamani ya bei ya hisa inapungua na kuchochea uuzaji wa hisa hizo ili kuepuka hasara. Hatua hiyo hufikia kikomo baada ya kupungua zaidi hadi pale wawekezaji wengi wanajitokeza kununua hisa hizo na kisha bei huanza kupanda tena.

**Bei ya Chini** ***(Low)***
Hii ndiyo bei ya chini zaidi iliyolipiwa hisa katika kipindi Fulani hususan katika kikao kimoja cha biashara.

***

**Wanahisa wasimamizi** ***(Majority Shareholder)***
Hawa ni wanahisa ambao wanasimamia nusu ya hisa za kampuni.

**Kubadili bei halisi ya hisa** ***(Manipulation {Price Manipulation})***
Hatua hii si halali kwani bei ya hisa huongezwa au kupunguzwa ili kuonyesha picha tofauti ya mauzo.

**Akaunti inayomilikiwa na dalali** ***(Margin Account)***
Akaunti hii hutumika kumkopesha mwekezaji pesa za ununuzi wa hisa.

**Kiwango cha mtaji wa soko au thamani ya mauzo** ***(Market Capitalization)***
Hiki ni kiwango cha jumla ya mauzo katika soko kinachopatikana baada ya kujumlisha na idadi ya hisa na bei ya sasa ya soko .

Kwa mfano , iwapo kampuni ina hisa milioni 10, na bei yake kwa kila hisa ni shilingi 10 kwa sasa, Kiwango cha mtaji wa soko cha kampuni hiyo kitakuwa shilingi milioni 100.

**Alama za soko** ***(Market Indices)***
ona **Index**

**Agizo la biashara ya haraka** ***(Market Order)***
Agizo hili hutolewa ili hisa zinunuliwe au ziuzwe kwa bei bora haraka iwezekanavyo.

**Sintofahamu kwenye soko** ***(Market Overhang)***
Hali hii ya soko hutokea wakati ambapo mauzo ya toleo jipya au hisa yamepungua kufuatia hatua ya wanunuzi kutarajia bei yake kurudi chini. Hivyobasi wanunuzi hawashiriki biashara hiyo na husalia waking'amua iwapo watanunua hisa hizo kwa wakati uliopo sasa au hapo baadaye.

**Bei ya soko** ***(Market Price)***
Bei hii ni ya mwisho kuripotiwa baada ya uuzaji wa hisa katika soko.

**Soko linalomilikiwa na kampuni** ***(Market Share)***
Kiwango cha soko kinachomilikiwa na kampuni dhidi ya washindani wake.

**Ushindani wa hisa sawia** ***(Matching Orders)***
Kitendo hiki si halali na kinahusu kupanga pamoja hisa zinazowiana kwa ununuzi au uuzaji ili zionekane kuwa

zinashiriki biashara kila mara.

**Habari za kampuni ambazo hazijatolewa kwa umma** ***(Material Information)***
Habari hizi hata hivyo huenda zikaathiri bei ya hisa za kampuni punde tu zinapotolewa hadharani. Kwa mfano kuna habari zinazohusu mipango ya upanuzi, matokeo ya kifedha na ununuzi wa kampuni.

**Tarehe ya kulipa hati za dhamana.** ***(Maturity Date)***
Hii ni tarehe ambapo kiwango kamili cha malipo ya ununuzi au uuzaji wa hati za dhamana kinafaa kulipwa mwekezaji. Tarehe hiyo inategemea maagizo ya kandarasi ya muda uliokubalika. Muda huo unapowadia, malipo kamili yasiyojumuisha malipo ya riba yanalipwa.

**Mwanachama** ***(Member)***
Huyu ni mwanachama wa soko la hisa hususan kampuni za udalali ambazo ni wanachama wa soko la hisa. Mwanachama ni lazima azingatie masharti na pia ni mmiliki wa viti katika soko la hisa.

**Muungano wa kuunda kampuni mpya** ***(Merger)***
Ushirikiano huu unahusu kampuni mbili au zaidi zinapoungana ili kuanzisha kampuni nyingine mpya kama njia moja ya kuimarisha hali ya utendaji kazi. Wanahisa wa kampuni zilizoungana wanapata fursa sawa ya umiliki wa hisa na manufaa mengine kutoka kwa kampuni mpya iliyozinduliwa.

Umiliki wa hisa chache zilizochini asilimia 50 ***(Minority Interest)***
Mwanahisa au kampuni zinaweza kumiliki hisa kadhaa lakini chini ya asilimia 50. Walio na hisa chini ya asilimia hii hawana uwezo mkubwa wa kudhibiti usimamizi wa shughuli za kampuni.

**Soko la mchanganyiko** ***(Mixed Market)***
Hili ni soko ambalo halina mwelekeo thabiti.

**Soko la fedha** ***(Money Market)***
Soko hili ni sehemu ya soko la mtaji na lilianzishwa kununua na kuuza bidhaa za kifedha za muda mfupi. Bidhaa zinazouzwa huvutia kiwango cha chini cha riba kama vile hewala za serikali.

**Hisa zinazouzwa kwa wingi** (Most Active)
Hisa hizi ndizo zilizouzwa kwa wingi katika soko la hisa kwenye kipindi Fulani. Wakati mwingi hisa hizi hushuhudia mauzo ya juu kwa siku.

**Hazina za uwekezaji wa pamoja** ***(Mutual Fund***
ona Collective Investment Schemes)

***

**Bidhaa za uwekezaji zisizo kuwa salama** ***(Naked Position)***
Huu ni umiliki wa hisa zisizoweza kuepuka madhara au hatari kwenye soko. Hata hivyo bidhaa hizi huwa na faida ya juu.
Wawekezaji wa reja reja hawashughuliki sana na bidhaa hizi ila wale wawekezaji wakuu ndiyo huonyesha haja.

**Kupunguzwa kwa muda wa mauzo** (Narrowing the Spread)
Hatua hii hudhihirisha kupunguzwa kwa muda wa bei ya ununuzi na uuzaji wa hisa. Muda huo unapopunguzwa ndiposa wanunuzi na wauzaji wengi hujitokeza na kisha hisa inakuwa maarufu na matokeo yake huwa bora.

**Soko finyu** ***(Narrow Market)***
Soko hili linashuhudia maombi finyu kutoka kwa wawekezaji na kusababisha kupungua kwa shughuli za kibiashara.

**Bidhaa za uwekezaji zenye faida ya chini** (Negative Carry
**ona** Positive Carry)

**Hisa zisizotosheleza** ***(Negative Equity)***
Hisa hizi hazitoshelezi kiwango cha mkopo uliochukuliwa kuwekezwa kwenye raslimali.

**Soko hafifu** ***(Nervous Market)***
Soko hili huathirika sana kutokana na mabadiliko ya kiuchumi au kisiasa.

**Thamani halisi ya hisa** ***(Net Asset Value)***
Hii ni thamani ya hisa moja ya hazina za pamoja na pia ile ya unit trust
Thamani hii hupatikana baada ya kuondoa bidhaa zenye hasara na kisha kugawanya na hisa zilizosalia.

**Mabadiliko kamili ya bei** ***(Net Change)***
Haya ni mabadiliko katika bei ya bidhaa za uwekezaji wa kifedha katika muda wa siku moja ikilinganishwa na siku iliyotangulia.
Mabadiliko yaweza kuwa na faida au hasara.

**Toleo jipya** ***(New Issue)***
Hii inahusu hisa au hati za dhamana zinazouziwa umma kwa mara ya kwanza.

**Makelele ya soko** ***(Noise)***
Makelele haya yanachochewa na kuyumbayumba kwa thamani ya kiwango cha biashara katika soko la hisa ambayo humchanganya mwekezaji huku akikosa kuelewa mwelekeo wa soko.

**Bei kamili ya bidhaa za kifedha za uwekezaji** ***(Nominal Value/ Face value)***
ona **Par Value.**

**Kampuni au mtu aliyeteuliwa kwa uhamisho wa hisa (Nominee)**
Jina hili hutumika kwa mtu au benki au dalali wa hisa aliyehamishiwa hisa au bidhaa zingine za uwekezaji ili kuendeleza shughuli za uuzaji na ununuzi.

**Akaunti teule** ***(Nominee Account)***
Akaunti ambayo dalali anashikilia hisa za wateja ili kurahisisha shughuli ya ununuzi na uuzaji.

***

**Kundi la hisa chache** ***(Odd Lot)***
Kundi hili la hisa linajumuisha hisa zilizo za kiwango cha chini ikilinganishwa na zile hisa zinazo hitajika katika mauzo. Katika soko la hisa la Nairobi, kundi hili la hisa linajumuisha hisa mia mbili au zenye thamani ya shilingi elfu moja.

**Bei ya chini (Offer)**
Hii ni bei ya chini zaidi ambayo mwekezaji angependa kuuza hisa zake

**Mgao wa faida uliosahaulika** ***(Omitted Divided)***
Mgao huu wa faida unatarajiwa na mwekezaji lakini haukuidhinishwa kwasababu za kifedha.kampuni huamua kuhifadhi mapato yake baada ya kulipa wanahisa.

**Kampuni iliyowazi na kuruhusu uwekezaji** ***(Open Ended Investment Company)***
Kampuni hii huzidi kukubalia wawekezaji wapya na kuwarejeshea malipo wale wangependa kuondoka. Kampuni hii inatofautiana na ile iliyo na idadi Fulani ya wawekezaji na haikubali wawekezaji wengine.

**Amri ya uuzaji na ununuzi wa hisa zilizofutiliwa mbali** ***(Open Order)***
Hii hutokea wakati ambapo bei iliyotarajiwa haijaafikiwa.

**Mfumo wa awali wa uuzaji na ununuzi** ***(Open Outcry)***
Mfumo huu wa kufanya biashara katika soko la hisa unajumuisha upazaji sauti baina ya madalai kuhusu hisa na bei za mauzo katika kipindi cha biashara.

**Uamuzi wa mwekezaji** ***(Option)***
Mwekezaji ana uwezo wakununua au kuuza hisa za kiwango fulani wakati uliokusudiwa.

**Kutowiana kwa hisa** ***(Order Imbalance)***
Hatua hii inahusu hisa za ununuzi zisizolingana na zile za uuzaji.

**Hisa za kawaida** ***(Ordinary Shares)***
ona **Shares.**

**Soko wazi** ***(Over the Counter{OTC})***
Soko hili halijumuishi soko la hisa la Nairobi bali biashara huendeshwa moja kwa moja baina ya madalali, wawekezaji na kampuni kupitia simu au mtandao wa internet.

**Hisa chache dhidi ya hitaji kubwa (Overheated Market)**
Tukio hili husababisha kuongezeka kwa bei ya hisa na linawashiria awamu ya kufanya vyema kwa soko. Pia linawashiria mwanzo wa awamu ya kushuka kwa bei hapo badaye.

**Maombi ya hisa kupita idadi iliyopo (Oversubscribed)**
Hitaji la hisa kwenye toleo la kwanza kwa umma huzidi idadi ya hisa zilizotolewa. Hatua hii hutokea wakati soko linafanya vyema, na pia wakati kuna toleo zenye kuvutia umma. ona **Hot Issue.**

**Thamani ya juu ya hisa isiyokuwa kamili** ***(Overvalued)***
Thamani ya juu ya hisa inapatikana iwapo thamani hiyo hailingani na viwango vingine vya uchunguzi vilivowekwa.

***

**Bei ya hisa dhidi ya mgao wa faida** ***(P/D Ratio)***
Hii ni bei inayolinganishwa na mgao wa faida. Unagawanya bei ya hisa dhidi ya mgao uliolipwa mwisho. Hii inasaidia kupata thamani halisi ya uwekezaji.

**Bei ya hisa dhidi ya mapato** ***(P/E Ratio)***
Bei hii hupatikana kwa kugawanya bei ya hisa katika soko  na mapato yaliyosajiliwa katika kipindi cha miezi kumi na mbili iliyopita.
Hii inaeleza jinsi bei ya hisa ilivyo ghali.
Kampuni zisizoandikisha faida hazina kiwango hiki na zile zilizo na kiwango cha juu zaidi huonekana kuwa hatarini.

**Jumla ya pesa zilizolipwa na mwekezaji** ***(Paid-up Capital)***
Kiwango hiki kinajumuisha idadi yote ya pesa zilizolipwa na wa wekezaji katika ununuzi wa hisa.

**Uuzaji wa ghafla** ***(Panic Selling)***
Hali katika soko la hisa ambapo mwekezaji anaingiwa na hofu na kuanza kuuza hisa zake bila kuzingatia bei, hatua ambayo huathiri bei ya soko.

**Hasara ya hewani au Hasara ambayo ingali kushuhudiwa** ***(Paper Loss)***
Hii hutokea wakati ambapo bei ya hisa kwenye soko ni ya chini ikilinganishwa na ilivyonunuliwa ingawa biashara yenyewe haijatimizwa. Hatua hii husababisha hasara ambayo haitambuliki hadi pale hisa zitakapouzwa. Hii ni hasara tu ya hewani.

**Faida ya hewani  au Faida ambayo ingali kushuhudiwa** ***(Paper Profit)***
Hatua hii hutokezea pale ambapo bei ya hisa kwenye soko imepanda ikilinganishwa na ilivyonunuliwa lakini biashara kamili haijafanyika. Hii husababisha kuwepo kwa faida ambayo haijashuhudiwa hadi wakati hisa hizo zitakapouzwa.

**Biashara isiyoshuhudiwa moja kwa moja** ***(Paper Trading)***
ona **Dry Run Portfolio.**

**Thamani kamili ya hati za dhamana** ***(Par Value)***
Kiwango cha fedha au thamani ya hati za dhamana ambayo hulipwa mwekezaji baada ya muda wa hati hiyo kukamilika.

**Kampuni kuu** ***(Parent Company)***
ona **Holding Company.**

**Kuegesha hisa kwa kusubiri uwekezaji m badala** ***(Parking)***
Mwekezaji anaweka rasilimali zake kwa bidha zilizo salama huku akitafuta njia badala za uwekezaji.

**Kuwasilisha baadhi ya hisa** ***(Partial Delivery)***
Hii ni wakati ambapo dalali anakosa kufuata maagizo ya kandarasi ya kufikisha hisa zote walizokubaliana na mteja. Kwa mfano yeye anapaswa kuwasilisha idadi ya hisa 1,000 lakini anawasilisha 800 pekee.

**Tarehe ya malipo** ***(Payment Date)***
Hii ni siku ambapo mgao wa faida uliotangazwa unalipwa.
Mgao huo hulipwa wanahisa wanaostahili pekee na ambao walinunua hisa kabla ya hisa hizo kuanza kuuzwa pamoja na mgao kwa soko la hisa.

**Kiwango cha malipo ya mgao wa faida** ***(Payout Ratio)***
Kiwango hiki kinaashiria kiwango cha mapato ya kampuni kilicho lipwa Kama mugao wa faida.

**Hisa za bei na mtaji wa chini zaidi** ***(Penny Stock)***
Hisa hizi ni za bei ya chini na wakati mwingi haziuzwi kwenye masoko ya hisa.

**Matokeo ya hisa** ***(Performance Stock)***
ona **Growth Shares.**

**Kundi la bidhaa tofautitofauti za uwekezaji (Portfolio)**
Kundi hili laweza kujumuisha hisa au hati za dhamana au hazina ya pamoja. Mteja anachagua kundi la bidhaa za uwekezaji kulingana na malengo yake na hali ya hatari.

**Bidhaa za uwekezaji zenye faida ya juu** ***(Positive Carry)***
Bidha hizi zina gharama ya chini na faida yake ni kubwa, kwa mfano unawezakuchukua mkopo wa shilingi 100,000 au laki moja unaotozwa riba ya asili mia 10 na kisha mkopo huu uwekeze katika hati za dhamana ili upokee faida ya asili mia 12.

**Hisa muhimu** ***(Pivotal Shares)***
Wakati mwingi hisa za kampuni kubwa na maarufu huonekana kuwa thabiti na bora. Soko linafuatwa mkondo wa hisa hizi wakati zinapopanda na kushuka.

**Ada ya ziada au ya juu au faida** ***(Premium)***
Kiwango kilicho ongezeka ikilinganishwa na bei halisi za uwekezaji.

**Ununuzi wa hisa kwa bei ya juu kutoka kwa wamiliki** ***(Premium Raid)***
Hii ni nafasi bora inayotolewa kwa kampuni kununua hisa kutoka kwa wanahisa lakini kwa bei ya juu ikilinganishwa na ile ya soko ili kuwavutia waweze kuuza.
Lengo la hatua hii ni kuchukua usimamizi wa kampuni.

**Bei ya kila mchango wa hisa** ***(Price Weighted Index)***
Alama hii hupatikana wakati kila hisa inapozingatiwa kulingana na mchango wake au uzito dhidi ya bei.

**Soko tangulizi** ***(Primary Market)***
Ni soko linaloshuhudia toleo la kwanza la hisa, hati za dhamana na mikopo. Katika soko hili bidhaa hizi zinanunuliwa moja kwa moja kutoka kwa muuzaji.

**Mbinu ya kibnafsi ya kukusanya mtaji** ***(Private Placement)***
Kampuni huuza hisa kwa wawekezaji wachache walioteuliwa hususan wawekezaji wa taasisi kupitia mbinu hii.

**Kubinafsishwa kwa kampuni** ***(Privatization)***
Hatua hii inahusu uuzaji wa hisa zinazomilikiwa na serikali kwa sekta ya kibnafsi.

Hutekelezwa kupitia toleo la kwanza au utoaji zabuni.

**Onyo kuhusu faida** ***(Profit Warning)***
Onyo hili hutolewa na kampuni ya umma mapema ili kueleza wanahisa wake kuwa haitarajii faida.

**Stakabadhi ya maelezo ya kampuni** ***(Prospectus)***
Stakabadhi hii rasmi, hujumuisha maelezo ya kampuni inayouza hisa kwa umma ili kumwezesha mwekezaji kufanya uamuzi ufaao.

**Ajenti halali na asiyekuwa mwanahisa wa kawaida** ***(Proxy)***
Ajenti huyu ameidhinishwa kisheria kumuakilisha mwanahisa wakati wa mikutano ya kampuni.

**Kampuni inayomilikiwa na umma** ***(Public Company)***
Kampuni hii tayari imeuzia hisa zake kwa umma kupitia toleo la kwanza na hisa hizo zinauzwa katika soko la hisa la Nairobi.

**Toleo la hisa kwa umma** ***(Public Offering)***
Ni kuuza hisa kwa umma na hufanyika kupitia toleo la kwanza la hisa na mbinu nyinginezo.
Kuna tofauti kati ya toleo hili na lile la kuuza hisa kwa wanahisa waliopo au rights issue au pia toleo la kibnafsi.

**Mkondo wa upungufu** ***(Pullback)***
Mkondo huu wa kupungua kwa bei kutoka ile ya juu zaidi huenda ni ishara ya kutarajia mabadiliko katika bei za hisa.

***

**Hisa zinazomilikiwa na wakurugenzi** ***(Qualifying Shares)***
Hizi ni hisa zinazopaswa kulipiwa na mtu yeyote anayetaka kuwa mkurugenzi kulingana na stakabadhi ya kanuni za kampuni.

**Idadi ya chini ya wanahisa** ***(Quorum)***
Kiwango hiki cha chini cha wanahisa kinahitajika ili kuidhinisha mapendekezo ya mkutano.

**Bei ya hisa kwa sasa wakati shughuli ya mauzo inapoendelea kwa soko la hisa.** ***(Quote)***

***

**Mwenye nia ya usimamizi wa kampuni** ***(Raider)***
Hatua hii inaashiria mtu binafsi au kampuni inayojaribu kununua hisa nyingi na zinazostahili kutoka kwa kampuni inayolengwa ili kuimiliki.

**Kipindi kinachozingatia kupanda au kushuka kwa bei ya hisa, hati za dhamana na hata alama ya kampuni bora** ***(Rally)***

**Ununuzi wa hisa nyingi** ***(Ramping)***
Ununuzi huu unafanyika ili kuinua hadhi ya kampuni na hisa zake na kisha kupelekea kupanda kwa hitaji na bei ya hisa.
**Faida ya malipo ya uwekezaji** ***(Rate of Return)***
Faida inayopatikana kutokana na jumla ya pesa zilizowekezwa.

**Pendekezo la mdadisi** ***(Rating {Stock Rating})***
Pendekezo hili huangazia iwapo hisa fulani zinafaa kununuliwa, kuuzwa au biashara hii isimamishwe kwa muda kufuatia kuatharika kwa matokeo.

**Msisimko kwenye soko la hisa** ***(Reaction)***
Hi hatua inayosababisha kipindi cha muda mfupi kuhusu mabadiliko ya bei ya hisa.
Soko linapopungua, hisa inaandikisha bei ya juu kwa muda mfupi na kisha soko linapopanda, bei ya hisa inapungua kwa kipindi kifupi.

**Kurejea kwa matokeo bora ya hisa** *(Rebound)*
Hii hutokana na hisa kuandikisha ongezeko la bei kwa muda baada ya kipindi cha upungufu.

**Mabadiliko ya kimtaji** *(Recapitalization)*
Mabadiliko haya yanatekelezwa ili kuleta mtaji mpya kupitia uuzaji wa hisa, hati za dhamana au mkopo.

**Kuwekwa chini ya mrasimu** *(Receivership)*
Kampuni inapofilisika inasimamiwa na kundi huru au meneja mrasimu anateuliwa kusimamia kampuni hiyo ili kupokea malipo ya madeni, anaposhindwa kuifufua basi inauzwa au kufungwa.

**Tarehe ya usajili** *(Record Date)*
Tarehe hii hutolewa na muuzaji ambapo wanahisa wanapaswa kujiandikisha rasmi ili kuweza kupata mgao wa faida au faida nyinginezo.

**Kiwango cha juu zaidi kinachoshuhudiwa kwa mara ya kwanza** *(Record High)*
Kiwango hiki cha bei kinaandikishwa wakati wa mauzo na kinalinganishwa na kiwango kama hicho cha awali.

**Kiwango cha chini zaidi kinachoshuhudiwa kwa mara ya kwanza** *(Record Low)*
Kiwango hiki ni cha chini zaidi kuafikiwa na hisa, hati za dhamana au bidha zinginezo.

**Msajili** *(Registrar)*
Msajili analo jukumu la kuhamisha hisa na kuziunganisha pamoja kwa niaba ya kampuni.

**Usajili wa wanahisa** *(Registration)*
Kampuni iliyoorodheshwa kwenye soko la hisa hutoa sajili ya majina na anwani za wanahisa na wakurugenzi. Kampuni zinapaswa kufanya hivyo ingawa wakati mwingi utaratibu huo hutumika kwa ajili ya kufanya mawasiliano na wanahisa.

**Kuwekeza faida** *(Reinvestment)*
Mwekezaji anaweza kuwekeza tena mgao wa faida, riba au faida nyingine kwa kukununua hisa badala ya kupokea pesa taslimu.

**Hatua ya mwanahisa kutotumia mamlaka yake Kwa kununua hati miliki ya hisa zilizotolewa wakati wa toleo hilo.** *(Renunciation)*

**Mwekezaji wa reja reja** *(Retail Investor)*
Mwekezaji huyu ananunua au kuuza kiwango cha chini cha hisa na kuhifadhi kwenye akaunti yake.

**Mapato yanayokusudiwa kufaidi kampuni** *(Retained Earnings)*
Mapato haya hayalipwi kama mgao wa faida bali husalia kuendeleza biashara au kulipa madeni.

**Mapato yanayohifadhiwa** *(Revenue Reserves)*
Mapato haya ni baadhi ya yale yanayoandikishwa na kampuni kama faida na hutumika kulipa wanahisa kama mgao wa faida au hutumika katika upanuzi wa kampuni.

**Kugawanya hisa kwa bei ya juu** *(Reverse Stock Split)*
Hatua hii husababisha kupungua kwa idadi ya hisa ambazo thamani yake na mapato hupanda. Hata hivyo mtaji wa kampuni haubadiliki.Kwa mfano hisa zinazogawanywa mara mbili zitapelekea Yule anayemiliki hisa 100 kwa shilingi 10 kuwa na hisa 50 kwa shilingi 20.

**Haki miliki** *(Rights Issue)*
Ni baadhi ya manufaa anayoshuhudia mwanahisa wa kampuni kwa kununua haki miliki za hisa kwa bei ya chini kabla kutolewa kwenye soko.

**Hatari iliyopo au inayotarajiwa** *(Risk)*
Hatua hii inahusu uwezekano wa kupata hasara na hutokea katika uwekezaji wowote.
Hata hivyo mwekezaji anapaswa kuzingatia swala hili na kulinganisha hatari iliyopo kati ya bidha mbali mbali za

uwekezaji kabla ya kufanya uamuzi.

**Kufahamu mapema** ***(Running Ahead)***
ona **Front Running.**

***

**Mauzo ya kila hisa** ***(Sales per Share)***
Jumla ya mapato yaliyopatikana kwa mwaka mmoja yakigawanywa dhidi ya idadi ya hisa. Kiwango hiki hutumika kuchunguza shughuli za kibiashara za kampuni.

**Hutumika kama stakabadhi ya umiliki wa hisa (Scrip)**

**Ukaguzi wa hisa** ***(Screening Shares)***
Hisa hufanyiwa ukaguzi ili kubaini zile zinazoafikia mahitaji ya kifedha na uwekezaji.

**Umiliki wa kiti katika soko la hisa** ***(Seat)***
Hii ni lugha ya kitambo inayomaanisha uanachama katika soko la hisa la Nairobi ili kushiriki katika biashara.

**Soko la upili** ***(Secondary Market)***
Hili ni soko ambalo wawekezaji hununua hisa na hati za dhamana kutoka kwa wawekezaji wengine mbali na kampuni iliyouza hisa kwenye toleo la kwanza
Soko la hisa na hati za dhamana la Nairobi ni soko la upili. Toleo la IPO hufanyika kwenye soko la utangulizi na kisha hisa hizo huuzwa katika soko la upili.

**Toleo la pili la hisa** ***(Secondary Offering)***
Toleo hili hutekelezwa na kampuni ambayo tayari imeshatoa hisa zake kwa umma hapo awali au kwa mara ya kwanza.
Toleo hili mara kwa mara hutekelezwa na kampuni zinazotafuta mtaji wa kujiendeleza.

**Sekta** ***(Sector)***
Sekta inaashiria kundi la bidhaa za uwekezaji kama vile hisa zinazouzwa kwa soko. Kundi hili lina sifa sawia kwa mfano kampuni za Kenya Airways na Uchumi Supermarket ziko chini ya sekta ya biashara na huduma ilhali Athi River Mining na Bamburi Cement ziko chini ya sekta ya ujenzi na washirika wake.

**Bidhaa za kifedha za uwekezaji** ***(Securities)***
Bidha hizi zinajumuisha hisa, hati za dhamana, mikopo, au hati nyinginezo zinazouzwa na serikali.

**Mauzo baada ya matokeo duni** ***(Sell Off)***
Hutokea wakati ambapo hisa au hati zinauzwa kwa wingi na kusababisha kupungua kwa bei. Hali hii hutokea wakati kampuni imeandikisha matokeo ya kughadhabisha.

**Matamshi na hisia za mwekezaji** ***(Sentiment)***
Hali hii yaweza kusababisha soko kupanda au kushuka

**Muda wa kugharamia bidhaa za uwekezaji** ***(Settlement Period)***
Huu muda unahitaji mnunuzi kulipia hisa alizonunua naye muuzaji anahitajika kuziwasilisha.

**Hisa (Shares)**
Kiwango cha umiliki wa sehemu ya kampuni.
Mmiliki wa hisa anaruhusiwa kumiliki sehemu ya kampuni na pia anapaswa kugawiwa faida zote za kampuni. Kuna aina tofautofauti ya hisa.

**Hisa za kawaida** ***(Ordinary Shares)***
Hisa hizi hazina masharti, zinampa mwekezaji umiliki kulingana na hisa anazomiliki kwenye kampuni. Zinampa mwanahisa mamlaka ya kuhudhuria mikutano, kupiga Kura na kupokea mgao wa faida.

**Hisa spesheli (Preference Shares)**

Hisa hizi zinapaswa kulipiwa mgao wa faida kila mwaka na mmiliki wa hisa hizi ndiye wa kwanza kulipwa mgao wa faida kabla ya  mmiliki wa hisa za kawaida.

**Hisa maalum zinazoweza kununuliwa tena** ***(Redeemable Preference Shares)***
Hizi ni aina ya hisa maalum ambazo zina mkataba wa maelewano. Kampuni yaweza kuzinunua tena baada ya muda wake kutimia kulingana na maagizo ya halmashauri.

Hisa maalum zilizo na uwezo wa kugeuzwa kuwa za kawaida wakati mmoja kulingana na masharti yaliyopo ***(Convertible Preference Shares)***

**Mtaji wa hisa** ***(Share Capital)***
ona **Authorized Share Capital.**

**Stakabadhi ya umiliki wa hisa** ***(Share Certificate)***
Ni stakabadhi inayoonyesha umiliki wa hisa. Inajumuisha thamani ya hisa, idadi ya hisa, nambari ya stakabadhi hiyo na jina la mmiliki.

**Mwanahisa** ***(Shareholder)***
Ni mtu au kampuni inayomiliki angalau hisa moja au zaidi za kampuni.

**Mpango wa kampuni kununua hisa zake** ***(Share Repurchase Plan)***
Mpango huu unawezesha kampuni kununua hisa zake tena kutoka kwa soko la wazi na hutokea wakati ambapo hisa za kampuni zimeuzwa kwa bei ya chini sana.

**Hisa zilizotolewa na kampuni na zinamilikiwa na umma (Shares Outstanding)**

**Uuzaji wa hisa zisizomilikiwa** ***(Short Sale {or Short Position})***
Uuzaji huu unaangazia hisa ambazo mtu yeyote hamiliki na muuzaji anatarajia kuzinunua tena kwa bei ya chini siku tofauti.

**Tofauti kati ya bei ya ununuzi na uuzaji** ***(Spread)***
Hali hii huchangiwa na hitaji la wateja na idadi ya hisa zilizotolewa.

**Agizo la Upigaji kura baina ya wanahisa kuwachagua wakurugenzi** ***(Statutory Voting)***
Kila mwanahisa anaruhusiwa tu kura moja kadri ya hisa anazomiliki. Kwa mfano iwapo anamiliki hisa 200 basi kura zake ni 200

**Hisa** ***(Stock)***
ona **Part One.**

**Soko la hisa** ***(Stock Exchange)***
Hili ni soko lililotengwa kwenye sehemu Fulani katika nchi ambapo biashara za uuzaji na ununuzi wa hisa zinaenelezwa. Pia hutumia mtindo wa kieletroniki.

Nchini Kenya soko la NSE ndilo soko pekee lililoidhinishwa.

***Stock Market***
ona **Part One.**

**Kipimo cha soko la hisa** ***(Stock Market Index)***
ona **Index.**

**Kugawanya hisa** ***(Stock Split)***
Hatua ya shirika au kampuni ya kugawanya hisa kuwa nyingi ambapo mwanahisa anapata hisa zilizogawanywa kulingana na zile anazomiliki katika kitabu cha usajili.

**Dalali wa hisa** ***(Stockbroker)***
Mtaalam anayenunua na kuuza hisa kwa niaba ya mteja katika soko la hisa.Yeye hulipwa ada kutokana na

shughuli hii na pia anatekeleza jukumu la kutoa ushauri kuhusu uwekezaji.

**Nembo ya hisa** ***(Stock Symbol)***
Ni nembo ambayo hupewa hisa fulani ili kushiriki katika biashara. Kwa mfano Kampuni ya Athi river mining ina nembo ya ARM, ilhali sasini tea & coffee nembo ya hisa zake wakati wa mauzo ni STC.

**Agizo la kusimamisha mauzo** ***(Stop Order)***
Agizo hili hutolewa na mwekezaji kwa dalali wa hisa likihitaji anunue au auze hisa kwa bei Fulani au bora zaidi.

**Agizo la jumla** ***(Stop-Limit Order)***
Agizo hili linajumuisha kusitisha au kupunguza uuzaji na ununuzi wa hisa kwa bei Fulani.

**Hisa inayoashiria habari muhimu za kampuni** ***(Story Stock)***
Hisa hizi hazielezi picha halisi ya mali za kampuni au mapato.

Kwa mfano bei ya hisa ya kampuni ya kilimo huenda ikaongezeka baada ya kutolewa kwa habari zinazohusu matarajio ya mavuno bora hapo baadaye.

**Pendekezo la hisa thabiti** ***(Strong Buy or Sell)***
Pendekezo hili hutolewa na mdadisi kwa mwekezaji kuwekeza kwenye kampuni fulani kufuatia matokeo bora au kusitisha shughuli kufuatia hali duni ya kiuchumi.

**Mbinu ya ufufuzi wa hisa zilizodorora** ***(Staying Power)***
Mbinu hii hutumika na mwekezaji ambapo anashikilia hisa zake licha ya bei kupungua kama mojawapo ya masharti ya uwekezaji katika soko la hisa. Mwekezaji hastahili kuwekeza pesa za hisa ambazo atazihitaji hapo baadaye.

**Wanaokopa ilihali sifa yao si bora** ***(Subprime)***
Wanaochukua mikopo na sifa zao zimeharibika. Jina hili lilipata umaarufu miaka ya 2007/2008 baada ya kutokea kwa msukosuko wa kifedha.

**Kutuma maombi ya ununuzi wa hisa kwenye toleo jipya** ***(Subscribe)***

**Toleo la pili na la baadaye la kuuza hisa kwa umma** ***(Subsequent Offering)***
ona **Secondary Offering.**

**Kusitisha biashara kwa muda** ***(Suspended Issue {Suspended Trading})***
Ni wakati ambapo biashara ya hisa za kampuni fulani inasitishwa kwa muda kufuatia hatua inayochukuliwa na soko la hisa. Hisa hizi haziwezi kuuzwa wala kununuliwa hadi sharti hili lifutiliwe mbali na soko la hisa.

**Hatari inayoambatanishwa na shughuli za soko** ***(Systematic Risk)***
Hatari hii hushuhudiwa na soko au sekta nzima kutokana na sababu za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

***

**Hatua ya Kampuni moja kununua nyingine** ***(Takeover)***
Huu ni wakati ambapo kampuni huchukua hatua ya kusimamia kampuni nyingine aidha kupitia mtindo wa kirafiki au kutumia mabavu.

**Bei inayolengwa na mwekezaji** ***(Target Price)***
Mwekezaji ananunua hisa akitarajia bei za hisa hizo zitaongezeka kufikia kiwango anachoazimia ili aweze kuuza hisa zake.

**Muda wa kulipwa kwa hati za dhamana** ***(Term to Maturity)***
Huu ni muda kati ya ununuzi wa hati za dhamana na wakati wa malipo ambapo Yule aliyeuza hati hiyo anapaswa kulipa pesa zilizogharimu hati hiyo na riba iliyopatikana. Wakati mwingi hati inayodumu kwa muda mrefu inavutia malipo ya faida ya juu na ile ya muda mfupi huvutia faida ya chini.

**Soko finyu** ***(Thin Market)***
Ni soko lililo na hisa chache za kuuza au kununuliwa . Shughuli finyu husababisha bei za hisa kuyambayumba zaidi.

**Kiwango cha mauzo** ***(Trade Volume)***
Hiki ni kiwango cha jumla ya hisa za kampuni zilizouzwa kwa kipindi fulani haswa katika mauzo ya siku. Kiwango hiki pia hutumika kwa idadi ya hisa zote zilizouzwa katika kipindi fulani.

**Ukumbi wa kuendesha biashara** ***(Trading Floor)***
Hii ni sehemu katika soko la hisa ambapo shughuli za ununuzi na uuzaji zinaendeshwa.

**Kusitishwa kwa biashara kwa muda** ***(Trading Halt)***
Hatua hii inamaanisha kusimamisha uuzaji wa hisa za kampuni fulani kwa muda kwenye soko la hisa.

Kutosawazishwa kwa hisa zilizohitajika na zile zilizopatikana, matatizo ya bei ya hisa kutofuatwa maagizo ndizo sababu za kusitisha biashara kwa muda

**Muda wa kuendesha biashara bora** ***(Trading Session)***
Biashara huendeshwa kwa siku baada ya kupigwa kwakengele ya ufunguzi na kukamilika baada ya kulia kwa kengele ya kutamatisha shughuli za siku.

**Hewala za serikali za muda mfupi** ***(Treasury Bill {T-Bill})***
Hizi ni hewala za serikali zinazodumu kwa mwaka mmoja au miezi kadhaa na zinauzwa kwa bei ya chini.

**Hati za dhamana za serikali** ***(Treasury Bond {T-BOND})***
Ni hati za dhamana zinazolipwa baada ya mwaka mmoja au zaidi na zinadhaminiwa na serikali. Anayemiliki hati hizi hupokea faida baada ya kila miezi sita almaarufu kama kuponi.

**Kuendesha biashara kwa imani** ***(Trust)***
Hii ni taratibu ya kisheria ambapo mwekezaji anampa mdhamini umiliki na usimamizi wa mali zake kwa manufaa ya wale wanaokusudiwa kufaidika na mali hizo.

**Kiwango cha thamani ya mauzo** ***(Turnover)***
Kiwango hiki kinajumuisha thamani ya hisa zilizouzwa kwa siku au kwa kipindi fulani cha biashara.

***

**Hisa zisizonunuliwa zote kupita kiwango cha chini kilichowekwa** ***(Undersubscribed)***
Hii hutokea iwapo maombi ya ununuzi wa hisa mpya ni kidogo mno. Kuna sababu nyingi za hali hii ikiwemo kutoamini ripoti inayotolewa kwa umma kuhusu kampuni husika, kutozingatia wakati ufaao na pia bei ya hisa isiyoridhisha.

**Hisa zenye thamani iliyokadiriwa kuwa ya chini kinyume na kiwango kamili** ***(Undervalued Shares)***
Hisa hizi huuzwa kwa thamani ya chini na isiyostahili. Kuna sababu kadhaa kama vile huenda sekta hiyo haijapigiwa upato na wakati mwingine kampuni husika haijulikani kwa wawekezaji na haija wavutia.

**Kampuni za kusimamia toleo au wadhamini** ***(Underwriters)***
Kampuni hizi spesheli hushughulikia toleo na kuhakikisha kuwa hisa mpya za kampuni zinawafikia wanahisa.

**Uwekezaji kwenye** ***Unit Trust***
ona **Collective Investment Schemes.**

**Hisa zisizoorodheshwa** ***(Unlisted Shares)***
Hizi ni hisa za kampuni ambazo hazijaorodheshwa katika soko la hisa kwa kutotimiza masharti yaliyowekwa. Hisa hizi huuzwa katika soko la wazi (OTC) baina ya dalali, wawekezaji na kampuni.

**Mgao wa faida ambao haujalipwa** ***(Unpaid Dividend)***

**Hasara ya hewani au haijashuhudiwa** ***(Unrealized Loss)***
ona **Paper Loss.**

**Faida ya hewani au haijashuhudiwa** ***(Unrealized Profit)***
ona **Paper Profit.**

***

**Kuwekeza kwa thamani ya hisa** ***(Value Investing)***
Ni mbinu ya kuwekeza kwa kampuni zenye hisa ambazo zinauza kwa bei iliyo chini ikilinganishwa na bei halisi.

**Mtaji wa kufadhili biashara geni** ***(Venture Capital)***
Huu ni mtaji unaokusanywa ili kufadhili shughuli geni za kibiashara.

**Hazina ya kusimamia pesa za kufadili wawekezaji** ***(Venture Capital Fund)***
Hazina hii ya uwekezaji inatunza pesa za wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwa hisa za kibinafsi ili kuanzisha biashara ndogo na za kadri.

**Hisa za kuyumbayumba** ***(Volatile Shares)***
Hizi ni hisa zilizo na uwezo wa kubadilika kutokana na kubadilika kwa bei katika kipindi cha muda mfupi

**Mamlaka ya kupiga kura** ***(Voting Right)***
Haya mamlaka yanamwezesha mwekezaji katika hisa za kawaida kupiga kura yeye mwenyewe au mwakilishi wake aliyeidhinishwa kuchagua bodi ya wasimamizi na maswala mengine ya sera. Idadi ya hisa inayomilikiwa inawakilisha idadi ya kura. Kwa mfano iwapo unamiliki hisa 1000, idadi ya kura ni 1000.

***

**Uhifadhi wa hisa za kampuni inayolengwa kumilikiwa (Warehousing)**
Utaratibu huu unawezesha kampuni moja Kwa mwendo wa polepole kuhifadhi hisa za kampuni nyingine ambapo kuna matarajio ya kuimiliki katika siku za usoni

**Ithibati ya umiliki wa hisa mpya** ***(Warrant)***
Hiki ni cheti kinachotolewa pamoja na hati za dhamana au hisa ambacho kinamwezesha mteja kununua hisa mpya kwa bei iliyokubaliwa. Cheti hiki hakina maana baada ya muda wake kumalizika.

**Mfumo wa kutumia tarakilishi yenye mtandao mkubwa** ***(Wide Area Network)***
Mfumo huu unamwezesha dalali kufikia soko la hisa na kufanya biashara kwenye afisi zao.

**Mbinu ya kufanya ulaghai katika biashara** ***(Window Dressing)***
Mbinu hii hutumika na baadhi ya taasisi za uwekezaji kama vile hazina za pamoja (mutual funds) ambapo zinauza hisa hafifu na zile thabiti kabla ya kutangaza kwa umma biashara zake ili kuonekana kuwa kampuni hizi zimekuwa zikishikilia hisa thabiti.

***

**Faida ya uwekezaji** ***(Yield)***
Malipo hayo yanatokana na kuwekeza kiwango Fulani cha hisa au hati za dhamana na huwakilishwa kwa asilimia.

Malipo hayo yanapatikana baada ya kugawanya mgao wa faida wa kila mwaka na bei ya hisa kwenye soko.

Kwa mfano hisa inayouza kwa shilingi 50 na mgao wa faida wa shilingi 5 kwa kila hisa utagawanywa na kutoa faida au malipo ya asilimia 10%

## SEHEMU YA TATU
## Habari zaidi kuhusu soko la hisa

**Jinsi ya kufungua akaunti ya CDS**

- Ni lazima kufungua akaunti ya CDS ili kununua au kuuza hisa za kampuni zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa la Nairobi.
- Unahitaji kumchagua ajenti wa kusimamia akaunti yako ya CDS. Ajenti huyu anaweza kuwa dalali au benki ya uwekezaji.
- Jaza na utie sahihi fomu yenye maelezo ya akaunti yako na utasaidiwa na ajenti uliyemchagua.
- Unahitajika kuwasilisha picha mbili ndogo ulizopigwa hivi karibuni.
- Wasilisha kitambulisho chako au pasi ya usafiri na nakala zake.
- Kampuni itahitaji kutoa cheti kamili cha maelewano pamoja na nakala yake.
- Ikiwa ni shirika lililosajiliwa kwa muundo tofauti kwa mfano lilisajiliwa kama chama fulani basi shirika hilo litahitajika kuwasilisha cheti cha usajili na nakala yake.
- Baada ya kujaza fomu ya usajili utaiwasilisha na kutia sahihi mbele ya ajenti wako.
- Utarejeshewa nakala ya fomu ya akaunti yako ili uihifadhi.
- Ajenti wako atakupa nambari ya akaunti ya CDS ambayo itabakia siri.
- Uko huru kufungua akaunti nyingine za CDS na madalali tofauti tofauti.
- Unaweza kuhamia kwa madalali wengine bora tu ujaze na kuweka saini fomu ya uhamisho. Fomu hii inapatikana kutoka kwa madalali na ni sharti dalali wa sasa na wa kitambo watie sahihi.

**Umuhimu wa kufungua akaunti ya CDS**

- Ni njia rahisi na salama ya kufanya biashara za hisa na hati za dhamana. Akaunti hii haichukuwi muda mwingi kama stakabadhi za makaratasi zilizokuwa zikitumika awali. Hisa zako huwekwa kwa akaunti baada ya siku tano za biashara.
- Siku za kufanya biashara zinapunguka na unapokea malipo kwa haraka.
- Kazi ya ziada ya matumizi ya karatasi sasa imefikia mwisho.
- Utumizi wa CDS umeondoa shida za kitambo ambazo zilizo kuwa zikisababisha hasara.
- CDS imepelekea kuimarika kwa soko na kupunguka kwa gharama ya kuendesha shughuli.

Mfumo wa kisasa wa akaunti za CDS, unasimamiwa na shirika la CDSC na ulianzishwa rasmi tarehe 10 mwezi Novemba mwaka 2004 baada ya kufutiliwa mbali matumizi ya karatasi.

**Umuhimu wa kuwekeza katika soko la hisa la Nairobi**

- Soko la hisa la Nairobi ni soko lenye usawa.
- Hisa zinazonunuliwa au kuuzwa katika soko la hisa zinaweza kubadilishwa na kuwa pesa taslimu kwa haraka.
- Bei ya hisa huamuliwa kwa usawa na uwazi chini ya mpango wa kuzingatia mahitaji na bidhaa zilizowasilishwa.
- Ni rahisi kuingia na kutoka katika soko hili. Masharti si mengi na unaweza miliki kampuni kwa sekunde.
- Bei ya hisa inaendelea kutangazwa mara kwa mara kwa manufaa ya mwekezaji
- Kuna aina nyingi za kampuni ambazo unaweza kuwekeza. Hii humwezesha mwekezaji kupanua uwekezaji wake.
- Hisa za kampuni nyingi katika soko la hisa mara kwa mara hulipa mgao wa faida na hivyo basi pesa za mwekezaji humfanyia kazi.
- Kuna habari tosha na sahihi kuhusu kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa hatua ambayo humwezesha mwekezaji kufanya uamuzi ufaao.
- Soko la hisa la Nairobi linawezesha kampuni kupokea mtaji na kujiimarisha.
- Mwekezaji analindwa vilivyo kufuatia kuwepo kwa sheria kali na thabiti katika soko.
- Soko thabiti la mtaji ni muhimu katika ustawi wa uchumi wa nchi.

**Jinsi ya kuanza biashara katika soko la hisa.**

Hisa zinaweza kununuliwa au kuuzwa na mtu yeyote ambaye ana pesa. Kufahamu maswala nyeti kuhusu soko kutakuwezesha kuelewa vyema jinsi soko hili linavyoendeshwa.

Watu walio na habari kuhusu soko hili ndio wanaweza kushamiri katika hii sekta ya uwekezaji. Idadi kubwa ya biashara hutekelezwa na madalali na hufanya biashara kwa niaba ya wawekezaji na pia hutoa ushauri mwafaka.

**1.Utafiti wa hisa**

Hili ni jambo la kawaida lakini ni gumu katika biashara ya hisa. Kwanza ni bora kuelewa vyema sekta unayotaka kuwekeza. Ukisha tambua ile sekta ungependa kuwekeza, unaweza sasa kuanzisha utafiti wa hisa.

**2. Uchunguzi wa historia ya hisa**

Wawekezaji wa muda mfupi wameelezea kutofahamu vyema historia ya hisa. Hata hivyo swala hili ni nyeti.

**3. Uchunguzi wa kiufundi**

Hii inahusu viashiria vya ustawi wa soko kama vile kiwango cha thamani ya mauzo na alama nyinginezo. Dalali wako atakuongoza katika uchunguzi wa kiufundi.

**4.Fuata maamuzi yako**

Ukisha kamilisha kutekeleza maamuzi kuhusu biashara ambayo ungependa kuendeleza hakikisha kuwa unazifuatilia kwa makini. Kwa mfano, kama biashara ni za muda mfupi au kipindi kirefu hakikisha kuwa unafuatilia kila mara biashara za kipindi kifupi ili kutafuta ishara za kujiondoa na zile biashara za muda mrefu zinaweza kuchunguzwa baada ya wiki, mwezi huku ukitelekeza miradi mengine. Unaweza kufuatilia matukio haya ya kibiashara kupitia vyombo vya habari ili kuelewa mapema jinsi hali ilivyo.

**5.Kufuatilia matukio ya sketa**

Unapaswa kuangazia sekta inayowakilisha hisa ulizonunua. Kwa mfano iwapo unatarajia bei kupanda kwenye sekta ya kilimo ambayo inajumuisha hisa unazomiliki na pia katika sekta hii kunazo hisa za kampuni nyingine ambazo bei imeimarika basi jua kwamba uamuzi wako ni mwafaka. Ukigundua kwamba mambo hayaendi sawa unaweza kuamua kujiondoa katika sekta hii baada ya kupokea faida.

**Jinsi bei ya hisa inavyobuniwa**

Idadi kubwa ya watu bado wamechanganyikiwa na jinsi bei ya hisa inavyoundwa wanapofuatilia matukio ya soko la hisa. Katika magazeti kuna wale wanaopatwa na mshangao kutokana na kupungua kwa bei ya hisa za kampuni maarufu ilhali kampuni
zisizo maarufu zinavutia bei ya juu zaidi.

Bei ya hisa wakati mwingine inatokana na imani ya mwekezaji inayochochewa na matokeo halisi au yanayotarajiwa. Uzito wa kampuni unaamuliwa na msingi wa kifedha na unaweza kuwaathirika kutokana na shughuli za uvumi zinazotolewa na mwekezaji.

Uvumi unaoenezwa katika soko la hisa huathiri hatma ya bei ya hisa, kwa mfano uvumi kuhusu upanuzi wa kampuni husababisha ongezeko la wawekezaji wanaotaka kununua hisa za kampuni hiyo.

Mtindo unaoangazia hisa zilizopo dhidi ya hitaji pia hutumika. Ongezeko la hitaji ya hisa litapelekea kupanda kwa bei na hofu kati ya wawekezaji husababisha upungufu kwa bei ya hisa, hata hivyo swala la thamani ya kampuni limebakia kuwa nyeti katika kutafuta bei ya hisa. Habari ya bei za hisa zaweza kupatikana kwenye maelezo mafupi ya magazeti ya kila siku au kupitia mtandao wa internet. Dalali wako wa hisa pia atakutumia ujumbe mfupi kupitia mtandao wa internet au simu

**Kuhusu ugawanyaji wa hisa**

Habari kuhusu kugawanywa kwa hisa ili kumwezesha mwekezaji kumiliki hisa nyingi zaidi, zimeenea katika soko la hisa na zimesalia kuwa hadithi. Licha ya mwekezaji kupata hisa nyingi baada ya kugawanywa, thamani ya kila hisa ziada wanayopokea inaendelea kupungua. Hata kama idadi ya hisa unazomiliki inaongezeka maradufu thamani ya awali inabakia jinsi ilivyo. Sababu zinazopelekea kampuni kugawanya hisa zinaegemea upande wa maswala ya hisia na saikolojia ya mwekezaji na hatua hii inamwezesha mwekezaji mdogo kununua hisa za bei ya kiwango cha juu. Kulingana na mwekezaji wa kima cha chini hisa zilizo ghali ni zile zinazouzwa kwa bei ya shilingi 100 na zaidi.

Ukweli uliopo kuhusu ugawanyaji wa hisa ni kwamba, hatua hii haiathiri matokeo ya kampuni na thamani ya hisa haibadiliki licha ya kumfurahisha mwekezaji kwa kumiliki hisa nyingi.

**Tofauti kati ya mitindo ya kibiashara ya upungufu na ongezeko wa soko la hisa**

Kuna mbinu mbili zinazoelezea hali ya soko ilivyo. Kuna mtindo wa ongezeko na ule wa upungufu. Mtindo wa upungufu unahusu kipindi kirefu cha kudorora kwa soko ilhali mtindo wa ongezeko unahusu kufanya vyema kwa soko kwa kipindi kirefu.

Wakati huu bei zinaweza kubadilika kwa kadri na kurejelea mitindo ya awali.

Hali ya kiuchumi ya nchi inaathiri mbinu hizi ambapo wakati kuna viwango bora vya riba na kiwango cha chini cha wasio na kazi soko huendelea kufanya vyema lakini soko hushuka wakati uchumi wa nchi umepata pigo na kampuni zinawafuta kazi wafanyikazi wake. Hii husababisha hofu kati ya wawekezaji.

Wakati wa mkondo wa kuimarika idadi ya wawekezaji inaongezeka na wengi wao wanauza hisa zao ili kuwekeza kwa bidhaa nyingine za uwekezaji.

Mahitaji yanaendelea kwenda chini , ongezeko la bidhaa linahuhudiwa huku bei ikipungua.

Katika mkondo wa upungufu, wawekezaji wananunua hisa nyingi kwa bei ya kuelewana na kufikia mwisho wa kipindi hiki wanafaa kujiandaa kushuhudia hasara kwa kipindi kifupi

**Tofauti baina ya hisa na hazina za pamoja**

Hazina za pamoja zinajumuisha ukusanyaji wa pesa kutoka kwa wateja wengi na kuwekezwa katika bidhaa tofauti tofauti kwa kusimamiwa na mtaalam. Uwekezaji katika bidhaa tofauti tofauti humlinda mwekezaji dhidi ya hasara inayotokana na biashara ya hisa. Iwapo kuna athari, itasambazwa kwa wawekezaji na kupunguza kiwango cha hatari kinachoshuhudiwa.
Wawekezaji wanaweza kufikia bidhaa nyingi tofauti chini ya uwekezaji wa pamoja.
Bidhaa hizi za uwekezaji zinajumuisha hisa, hati za dhamana na bidhaa zinazouzwa katika soko la fedha. Uwekezaji huu una changamoto zake. Bali na kugharamia ada inayotozwa, mwekezaji hana mamlaka ya kufanya uamuzi yeye mwenyewe na mapato halisi ya soko la hisa hayawiani kikamilifu na yale yanayopatikana katika hazina ya pamoja.

**Habari zaidi kuhusu uwekezaji;**
**Nini sababu za kuwekeza?**
Unapaswa kuwekeza ili pesa zako ziongezeke na kukabiliana na kupanda kwa mfumko wa bei. Haijalishi kama umewekeza pesa zako kwa hisa, hati za dhamana au hati nyinginezo, bali swala muhimu ni kubuni mali kwa manufaa ya uzeeni, ndoa, karo n.k.

**Ni lini unapaswa kuweweza?**

Ni bora kuanza kuwekeza mapema. Hali hii ina hakikisha kuwa uwekezaji unaimarika kwa muda ufaao na kuzalisha riba ya juu kwa mapato, maswala haya matatu yanapaswa kuzingatiwa na wawekezaji.
1.Unapaswa kuwekeza mapema
2.Wekeza kila mara
3.Wekeza kwa kipindi kirefu wala si kwa muda mfupi
Ni vyema kuanza kuwekeza mapema na kuwa na subira huku ukiimarisha uwekezaji wako kwa ajili ya kupata fedha nyingi hapo baadaye. Hii ndiyo sababu hisa ni bora za kuwekeza kwa kipindi kirefu. Kuimarika kwa uchumi kunazuia kupunguka kwa soko la hisa na athari ya kushuhudia hasara.

**Ni kiwango kipi unapaswa kuwekeza?**
Hakuna kiwango fulani kinachohitajika kuwekezwa na mwekezaji ili kupata faida. Kiwango unachoweka kinafaa kuzingatia maswala haya:
1.Hatari iliyopo
2.Muda wa uwekezaji
3.Akiba zilizopo
Kumbuka kwamba hakuna kiwango kidogo cha pesa ambacho hakifai kuwekezwa. Kiwango chochote cha pesa ulizonazo kinatosha kuanzisha uwekezaji wowote na unaweza kuimarisha uwekezaji kwa kipindi fulani unapopata kuelewa vyema nafasi zilizopo za uwekezaji.
Badala ya kuendelea kuota na kusubiri muda ufaao anza kuwekeza haraka iwezekanavyo kwa kutumia pesa ulizohifadhi.

**APENDIX 1**
**Wanachama wa soko la hisa na hati za dhamana la Nairobi (NSE) na chama cha Kenya cha madalali wa hisa na benki za uwekezaji (KASIB)**
**(Kufikia mwezi wa Agosti mwaka 2013)**

1. ABC Capital Ltd
2. African Alliance Investiment Bank
3. AIB Captial Limited
4. Apex Africa Investiment Bank
5. CfC Stanbic Financial Services
6. Francis Drummond & Co. Limited
7. Dyer And Blair Investiment Bank
8. Faida Investiment Bank
9. Genghis Capital Ltd
10. Kestrel Capital
11. Kingdom Securities Ltd
12. NIC Capital Securities
13. Old Mutual Securities Limited
14. Renassance Capital
15. Standard Investiment Bank

16. Sterling Investiment Bank
17. Suntra Investiment Bank
18. Francis Thus & Partners Limited
19. Shah Munge & Partners Limited
20. Ngenye Karuiki & Co. Ltd (Under statutory management)
21. Discount Securities Limited (Under statutory management)
22. Nyaga Stockbrokers Limited (Under statutory management)

**APENDIX 2**

**ALAMA YA KAMPUNI BORA 20 KWENYE SOKO LA HISA (NSE 20 SHARE INDEX**

**(Kufikia mwezi Agosti mwaka 2013)**

Kampuni hizi 20 zimeorodheshwa kwenye soko bila ya kufuatwa orodha yoyote:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Kakuzi Ltd | Kilimo |
| 2. | Sasini Ltd | Kilimo |
| 3. | Barclays Bank of Kenya | Benki |
| 4. | Equity Bank | Benki |
| 5. | Kenya Commercial Bank | Benki |
| 6. | Standard Chartered Bank | Benki |
| 7. | The Co-operative Bank | Benki |
| 8. | Kenya Airways | Biashara na Huduma |
| 9. | Nation Media Group | Biashara na Huduma |
| 10. | ScanGroup | Biashara na Huduma |
| 11. | Uchumi | Biashara na Huduma |
| 12. | Athi River Mining | Ujenzi na washirika wake |
| 13. | Bamburi Cement | Ujenzi na washirika wake |
| 14. | Kengen | Kawi na maafuta |
| 15. | KENOL | Kawi na mafuta |
| 16. | Kenya Power & Lighting Co Ltd | Kawi na mafuta |
| 17. | British American Tobacco | Utengenezaji bidhaa na washirik wake |
| 18. | East African Breweries Ltd | Utengenezaji bidhaa na washirika wake |
| 19. | Mumias Sugar | Utengenezaji bidhaa na washirika wake |
| 20. | Safaricom Ltd | Teknolojia ya mawasiliano |

**APENDIX 3**

**KAMPUNI ZOTE ZILIZOORODHESHWA KWENYE SOKO LA HISA NA HATI ZA DHAMANA (THE NSE ALL SHARE INDEX)**

**(Kufikia mwezi Agosti mwaka 2013)**

**SEKTA YA KILIMO**

1. Eaagads Ltd
2. Kapchorua Tea
3. Kakuzi Ltd
4. Limuru Tea Co. Ltd
5. Rea Vipingo Plantations Ltd
6. Sasini Ltd
7. Williamson Tea Kenya Ltd

**BISHARA NA HUDUMA**

1. Express Ltd
2. Kenya Airways Ltd
3. Nation Media Group
4. Standard Group Ltd
5. TPS Eastern Africa (Serena) Ltd
6. Scangroup ltd
7. Uchumi Supermarket Ltd
8. Hutchings Biemer Ltd

9. Longhorn Kenya Ltd

**TEKNOLOJIA YA MAWASILIANO**

1. AccessKenya Group Ltd
2. Safaricom Ltd

**MAGARI NA BIDHAA ZAKE**

1. Car and General (K) Ltd
2. CMC Holdings Ltd
3. Sameer Africa Ltd
4. Marshalls (E.A.) Ltd

**BENKI**

1. Barclays Bank Ltd
2. CFC Stanbic Holdings Ltd
3. I&M Holdings Ltd
4. Diamond Trust Bank Kenya Ltd
5. Housing Finance Co Ltd
6. Kenya Commercial Bank Ltd
7. National Bank of Kenya Ltd
8. NIC Bank Ltd
9. Standard Chartered Bank Ltd
10. Equity Bank Ltd
11. The Co-operative Bank of Kenya Ltd

**BIMA**

1. Jubilee Holdings Ltd
2. Pan Africa Insurance Holdings Ltd
3. Kenya Re-Insurance Corporation Ltd
4. CFC Insurance Holdings
5. British-American Investments Company (Kenya) Ltd
6. CIC Insurance Group Ltd

**UWEKEZAJI**

1. Olympia Capital Holdings Ltd
2. Centum Investment Co Ltd
3. Trans-Century Ltd

**UTENGENEZAJI BIDHAA NA WASHIRIKA WAKE**

1. B.O.C Kenya Ltd
2. British American Tobacco Kenya Ltd
3. Carbacid Investments Ltd
4. East African Breweries Ltd
5. Mumias Sugar Co
6. Unga Group Ltd
7. Eveready East Africa Ltd
8. Kenya Orchards Ltd
9. A. Baumann Co. Ltd

**UJENZI NA WASHIRIKA WAKE**

1. Athi River Mining Ltd
2. Bamburi Cement Ltd
3. Crown Berger Ltd
4. E.A. Cables Ltd
5. E.A. Portland Cement Ltd

**KAWI NA BIDHAA ZA MAFUTA**

1. KenolKobil Ltd

2. Total Kenya Ltd
3. KenGen Ltd
4. Kenya Power & Lighting Co. Ltd

**KITENGO CHA UKUAJI WA BIASHARA**

1. Home Afrika Ltd

**Apendix 4**

**VITENGO VYA SOKO**

1. Kitengo kikuu cha uwekezaji (MIMS)
2. Kitengo mbadala cha uwekezaji (AIMS)
3. Kitengo cha ukuaji wa biashara (GEMS)

**BACK COVER**

SOKO LA HISA NA HATI ZA DHAMANA LA NAIROBI (NSE)
Jumba la The Exchange, barabara ya Westlands 55,
P.O. BOX, 43633 - 00100, Nairobi.
Nambari ya Simu: +254 20 2831000
Barua pepe: info@nse.co.ke
Website: www.nse.co.ke

CHAMA CHA KENYA CHA MADALALI NA BENKI ZA UWEKEZAJI (KASIB)
Jumba la City, orofa ya sita, barabara ya Wabera,
P.O. Box, 43593-00100, Nairobi.
Nambari ya Simu : +254 20 2371470
Barua pepe: info@kasib.co.ke
Website: www.kasib.co.ke